SUPA JACKPOT
TZS.1,087,305,640
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MWAKILISHI** wa Nipashe Kanda ya Ziwa afariki dunia




UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Machi 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581244
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Samia: Sibagui, wote ni wangu

UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo ya maridhiano kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, aliyeikabidhi kwa niaba ya Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), baada ya kuwahutubia kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mjini Moshi, Kilimanjaro jana. **PICHA: IKULU**

## ...Mbowe asema kuna wahafidhina wasioitakia mema Tanzania

UKURASA 2



## Wanawake wa The Guardian wawakumbuka wagonjwa Mwananyamala

UKURASA 3

Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, linalochapishwa na Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Beatrice Bandawe (wa tatu kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa Ofisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Dar es Salaam jana, vilivyotolewa na kampuni hiyo ili kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. Wengine ni Mhariri wa Habari wa gazeti hilo, Salome Kitomary (kushoto), Ofisa Utawala wa TGL, Rehema Shedrack na baadhi ya wafanyakazi wanawake wa kampuni hiyo. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: MIRAJI MSALA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DIVISHENI YA BIASHARA**
**ILIYOPO DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 90 OF 2022**
**ALTAS YAG SU VE TARIM URUNLERI GIDA INSAAT OTOMOTIVE NAKLIYAT SANAYI VE TICARET A.S......MDAI**
**DHIDI YA**
**OSMANLI BUILDING CENTRE COMPANY LIMITED..............................MDAIWA.**

**KUITWA SHAURINI**

**KWAKO:**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**OSMAN BUILDING CENTRE KAMPUNI LIMITEDI**
**S.L.P 13851,**
**DAR ES SALAAM.**

**POPOTE ULIPO:** Mdai amefungua kesi dhidi yako juu ya malalamiko yake katika mahakama hii, na mahakama imeamuru kutoa amri ya kukuita katika shauri kwa kutoa amri ya kuchapisha mbele ya gazeti hili. Mahakama imeamuru ukachukue kopi ya nyaraka za shauri hili kwenye masijala ya Mahakama hii, S.L.P. 12533, Dar es Salaam. Unatakiwa kufika katika Mahakama hii wewe binafsi au Wakili wako au Mwakilishi yoyote wa kampuni hii tarehe 20/03/2023 saa 03:00 Asubuhi mbele ya Mh. Jaji A. Mbangwa, kupokea amri za mahakama.

Zingatia ukishindwa kufika mahakamani kama ilivyoelekezwa, shauri hili litaendelea na maamuzi yatatolewa bila uwepo wako.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA BIASHARA**
**DAR ES SALAAM**

**MICHEZO** **SIMBA KUBADILISHA GIA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), akizungumza na wafanyakazi wa benki hiyo, katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia: Sibagui, wananchi wote wangu

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema hakusita kukubali alipopata mwaliko wa kuwa mgeni rasmi katika kongamano la Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) kwa kuwa yeye ni kiongozi wa Watanzania wote.

Akizungumza jana katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo kitaifa yaliandaliwa na BAWACHA na kufanyika katika Manispaa ya Moshi, Rais Samia alisema anatambua nafasi aliyo nayo na kwamba hana ubaguzi wa aina yoyote.

"Nilipopata mwaliko wa kuja kwenye maadhimisho haya, sikusita kwa sababu nikiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kundi hili ni kundi langu pia. Huwezi kuitwa na wananchi wako ukasema siji. Haiwezekani.

"Lakini nilifurahi kuja pia kwa sababu nilijua kwa sababu nitasikia CHADEMA wanasema nini na kwa kweli nimesikia wanawake wa CHADEMA wanasema nini, CHADEMA wanasema nini, kama chama kinasema nini," alisema.

Rais Samia pia aliwataka CHADEMA na BAWACHA panapotokea hoja, wakae wazungumze na si kupayuka kwenye majukwaa na kuanza kushambuliana.

"Tusibomoe taifa letu kwa hali yeyote ile. Hakuna kisichowezekana kwenye mazungumzo. Tumeshuhudia nchi kadhaa zikiingia kwenye vita, hakuna kupata suluhu. Suluhu ilipatikana kwenye mazungumzo.

"Kwa hiyo tuendelee kuzungumza. Najua si rahisi kabisa watu kuja na utamaduni huu mpya ukakubalika mara moja. Si rahisi, kwangu kuna vikwazo, kwenu kuna vikwazo. Kwa Tanzania nzima, kwa pande zote si rahisi kukubali utamaduni huu mpya kwa haraka.

"Lakini wakiona matunda yaliyotokea utamaduni utakubalika. Hakuna mwanadamu kaumbwa anapenda vurugu tu, fujo, hakuna. Kila mwanadamu anapenda amani ya roho yake kwa hiyo twendeni tujenge amani ya nyoyo zetu," alisisitiza.

Rais Samia alisema CHADEMA haina dhamira ya kushika dola mwaka 2025 kwa kuwa wanajua yeye (Samia) yupo.

"Hamna dhamira ya kushika dola 2025. Hamna. Mnajua mama yupo. Mnajua mama yupo, dhamira hiyo haipo. Lakini yes (ndiyo) niseme wote tuna lengo hilo, lakini tukafanye kwa ustaarabu kama watu.

Tuheshimiane na nchi yetu iheshimike duniani.

"Nataka kuwaambia kwa kipindi hiki kifupi nchi yetu inaheshimika sana duniani, sana sana duniani. Kwa hiyo tusiirudishe chini, tusiirudishe nyuma. Twendeni na mwendo huu, tuweke heshima ya nchi yetu pale inapostahili. Tanzania ni taifa kubwa tusilitolee sifa yake," alisema.

**MAADHIMISHO KISIASA**

Rais Samia katika hotuba yake, alisema sura ya baraza hilo kwa jana ilikuwa ya kisiasa zaidi na kwamba anaamini atapata jukwaa lingine aseme yale yote ambayo serikali yake imeyafanya ndani ya kipindi cha miaka miwili ambacho amekuwa kiongozi wa nchi.

"Lilinijia wazo tufanye maridhiano, tuvumiliane. Yamesemwa mengi na mimi leo nimefurahi sana Mwenyekiti Mbowe hapa kwamba amesema sisi CHADEMA tumewafundisha watu wetu 'no hate no fear' (hakuna chuki hakuna woga). Hatuna haja ya kulipiza kisasi, nimefurahi sana.

"Niwaahidi ndugu zangu mageuzi yapo na tutajenga taifa jipya. Taifa la Tanzania lenye ushindani wa kisiasa, bila vurugu. Huko ndiko tunakotaka kwenda.

"Nimewasikia, unajua wakati nilipopendekeza kwenye chama changu tufungue mikutano ya hadhara kulikuwa kugumu kidogo, mjadala ulikuwa mkubwa kidogo. Kama ninyi juzi mlikuwa na mjadala kidogo, kwa nini mmemuita Rais kwenye hili jukwaa. Kwa hiyo Mwenyekiti (Mbowe) wale wahafidhina wako kwangu wako kwako," alisema.

"Wako waliomwambia Mbowe umeshalishwa asali, tuambie Ikulu siku uliyotolewa jela umekwenda kuambiwa nini, mbona umekuja na 'tone' hii sasa hivi. Akienda nje anatandikwa anaambiwa jamani sitaki kurudi kule mwendo ni huu huu kama tunavyofanya kwa hiyo wahafidhina watatuelewa jinsi matokeo yanavyokuja.

"Ndugu zangu siasa ni mchezo wa fikira na mawazo, kulumbana kwa hoja kuangalia kakosea wapi ni mzodoe na mimi naona kasema nini namjibu," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema wataendelea kutekeleza wajibu wao kama wapinzani kuishughulikia serikali yake kikamilifu na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Mheshimiwa Rais, bila hofu wala bila woga lakini tutafanya yale yaliyo sahihi, yaliyo na uhakika, yaliyo na ushahidi ili sio tu muweze kunyoosha nchi lakini na sisi tuweze kupata nafasi ya kuongoza siku za usoni.

"Ni matumaini yangu mheshimiwa Rais, azma yako ya kuliweka taifa pamoja litarithiwa na viongozi walioko chini yako, walioko katika serikali yako, katika taasisi mbalimbali za utoaji haki katika nchi yetu.

"Mheshimiwa Rais, demokrasia haipaswi kuwa chaguo yaani 'option', hakuna taifa lililopuuza demokrasia likakumbatia mifumo yenye udikteta, uonevu na dhambi likastawi. Tunapaswa wakati wote kuwa na viongozi wenye hofu ya kweli, ya Mungu na siyo ya uigizaji," alisema.

Kuhusu katiba mpya, Mbowe, alimwomba Rais Samia kuongeza wigo wa maridhiano akieleza,

"Naomba nisisitize jambo moja muhimu litakalorasimisha maridhiano yetu katika taifa na ni katiba mpya na katiba bora. Mheshimiwa Rais na vyombo vyako vyote nawasihi sana msipuuze kauli hii.

"Msione ni kauli ya utani, msione ni kauli ambayo inaweza ikapuuzwa. Kauli hii naomba muichukue kwa uzito mkubwa, ndio kilio na sauti ya taifa," alisema na kuongeza:

"Mheshimiwa Rais ulisema unakwenda kuunda chombo cha kushughulikia katiba, muda umeshakwenda ni miezi miwili, tunatambua majukumu makubwa yanayokukabili lakini vilevile, ona jambo hili nalo linahitaji umuhimu wa kipekee tuweze kutengeneza chombo hiki cha kuleta watu pamoja na tuanze kuweka mifumo sahihi ya kuipata katiba yetu."

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha**

## ...Mbowe asema kuna wahafidhina wasioitakia mema nchi

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema yawezekana ndani ya serikali kuna wahafidhina wanaotamani kukwamisha maridhiano au mchakato wa kuipata Katiba mpya ikiwamo Tume Huru ya Uchaguzi.

"Hawa siamini kwamba wanaitakia mema nchi yetu. Nakusihi, nakusihi, usikubali dhambi hiyo, kwani adhabu yake atoaye Mungu wetu, hatutamani, wala hatuombi imkute mtu yeyote katika taifa letu.

Mbowe alisema hayo jana katika kongamano la BAWACHA, alipokuwa akimkaribisha Rais Samia Suluhu Hassan.

"Sisi kama CHADEMA tuko tayari kusamehe na kusahau tulikotoka kwa sababu mheshimiwa Rais umeonyesha roho nyepesi, roho ya wazi, roho safi ya kuibadilisha na kujutia huko tulikotoka."

Akizungumzia suala hilo Rais Samia alisema, juzi CHADEMA walikuwa na mjadala kidogo, wa kwanini wamemuita (Rais). "Kwa hiyo Mwenyekiti (Mbowe), wale wahafidhina wako kwangu, wako kwako. Wako waliomwambia Mbowe umeshalishwa asali, tuambie Ikulu siku uliyotolewa jela umekwenda kuambiwa nini, mbona umekuja na toni hii sasa hivi."

"Akienda nje anatandikwa, anaambiwa jamani sitaki kurudi kule. Mwendo ni huu huu kama tunavyofanya. Kwa hiyo wahafidhina watatuelewa jinsi matokeo yanavyokuja.

"Ndugu zangu siasa ni mchezo wa fikira na mawazo, kulumbana kwa hoja kuangalia kakosea wapi nimzodoe na mimi naona kasema nini, namjibu.

Kuhusu maridhiano, Rais Samia, alisema katika mchakato huo, CHADEMA kilimwomba kuwasikiliza na kwa kuwa haikuwa rahisi alimwagiza Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdurahman Kinana achague watu watano na Mwenyekiti CHADEMA (Mbowe), apeleke watu watano wakae wazungumze.

"Niwaombe hapa mlisema never, never, niwaombe sana wezangu wanasema it takes too tangle. "Sasa ndugu zangu, acheni yale tusivutane. Taifa letu libaki salama. Ile never never again na mimi naiunga mkono."

Vilevile, Rais Samia amewataka BAWACHA kufanya siasa za kistaarabu akisema, "Ndugu zangu wa BAWACHA, twendeni tukafanye kazi kwa pamoja kukuza teknolojia, kukuza uchumi wetu, kustawisha jamii yetu ya kitanzania, lakini kama alivyosema Mwenyekiti wa BAWACHA na Mwenyekiti wa CHADEMA, kukuza siasa zetu pia, lakini za kistaarabu za maelewano."

Awali akitoa salamu za BAWACHA, Katibu Mkuu wa Baraza hilo, Catherine Ruge, alisema wanawake wanajua wanaomkatisha tamaa Rais Samia ni wanaume, lakini asijali BAWACHA iko nyuma yake.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA na Mwenyekiti wa BAWACHA Kilimanjaro, Grace Kiwelu, alisema Rais Samia na Freeman Mbowe, wamebadilisha kabisa siasa za Tanzania, kamati ya maridhiano inaenda kumaliza siasa za ubaguzi, kunyang'anywa ushindi, kunyimwa uhuru wa kukusanyika na kwamba wanaofanya hivyo ni wanufaika wa moja kwa moja.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha**

HABARI KITAIFA

# Wanawake Guardian wawakumbuka wagonjwa Hospitali Mwananyamala

**Na Elizabeth Zaya**

WANAWAKE wa Kampuni ya The Guardian Ltd jana walisherehekea Siku ya Wanawake Duniani kwa kutoa zawadi mbalimbali kwa wagonjwa waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala.

Zawadi hizo zilitolewa kwenye wodi za wanawake waliojifungua, wajawazito, wasiojiweza na wazee waliolazwa katika hospitali hiyo.

Miongoni mwa zawadi zilizokabidhiwa ni doti za kanga, pampers, sabuni, taulo za kike pamoja na katoni za maji ya kunywa ya Kilimanjaro. Wanawake wa The Guardian Ltd, walifika katika hospitali hiyo asubuhi na kupokewa kwa shangwe na kundi la wafanyakazi wanawake wa hospitali hiyo. Kabla ya kuanza kugawa zawadi zao katika wodi mbalimbali, walikaribishwa katika eneo maalumu kwa ajili ya utambulisho mbele ya kundi la wanawake mbalimbali waliokuwa wamejipanga kuona wagonjwa katika hospitali hiyo na kisha kuongozwa na kundi hilo kuelekea katika wodi hizo kwa ajili ya kugawa zawadi kwenye wodi nne za wajawazito na wagonjwa wa kawaida.

Akizungumza baada ya kukabidhi zawadi hizo, kiongozi wa msafara wa wanawake wa The Guardian Ltd, Beatrice Bandawe, alisema katika siku hiyo muhimu waliona ni muhimu kuungana na wagonjwa hao ili wajione ni sehemu ya wanawake wenzao na kuwapa faraja.

"Kwa niaba ya wanawake, wafanyakazi wa The Guradian Ltd chini ya IPP Media, tumependa kusherehekea siku hii ya wanawake, kwa kuwakumbuka wanawake wenzetu ambao wengi wao wanapitia machungu labda ya kujifungua au kuugua magonjwa mbalimbali, tumeona tusherehekee nao kwa kuwaletea kitu kidogo tulichojaliwa ili nao wafarijike katika siku hii muhimu kwa wanawake wote."

"Tunashukuru sana Hospitali ya Mwananyamala wametupokea vizuri, Mungu awabariki sana kwa kazi yenu nzuri mnayoifanya."

Muuguzi Kiongozi wa wodi ya wanawake katika hospitali hiyo, Mwanahija Biamwale, alisema zawadi zilizotolewa kwa wagonjwa ni jambo jema na la kupongezwa kwa sababu zinachangia kuleta faraja kwao na kwa wagonjwa pia.

"Kwa niaba ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, tunayo furaha kubwa sana kwa ujio wenu ndugu zetu wa The Guardian Ltd, kwa zawadi nyingi ambazo mmewaletea wagonjwa wetu kuwafariji, kwa kweli tumefurahi sana na sisi kwa sababu furaha ya wagonjwa wetu ni furaha yetu sisi watoa huduma," alisema Mwanahija.

"Tunajijua kabisa tuko hapa kwa ajili yao na ninyi mmekuja kuungana nasi ili kuwafariji, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu pale ambapo mmetoa, Mungu akajaze zaidi. Tunawaombea afya njema, tunawaombea kazi njema, maisha yenye furaha ili mwakani tukutane tena, karibuni sana Mwananyamala Hospitali na asanteni kwa kuja."

# Mwakilishi wa Nipashe Kanda ya Ziwa afariki dunia

**Na Waandishi Wetu**

MWANDISHI Mwandamizi wa magazeti ya Kampuni ya The Guardian Ltd Kanda ya Ziwa, Richard Makore amefariki dunia kwa ajali ya gari.

Makore aliyekuwa Mhariri wa Kanda ya Ziwa, alifariki dunia katika ajali ya basi la Kampuni ya Sheraton lenye namba za usajili T 922 ADC iliyotokea juzi katika Kijiji cha Mwilima, Kata ya Kasamwa, mkoani Geita.

Ajali hiyo ilitokea baada ya tairi la mbele kuchomoka na kusababisha basi hilo kutumbukia mtaroni wakati likitokea mkoani Mwanza kwenda Ushirombo wilayani Mbogwe, mkoani Geita.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Berthaneema Mlay, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo ambayo watu tisa walifariki dunia na zaidi ya 30 kujeruhiwa.

Mlay alisema dereva wa basi hilo alipoteza ustahimilivu baada ya tairi ya mbele kupasuka na hivyo kwenda kutumbukia darajani.

Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Geita na majeruhi walipelekwa katika Kituo cha Afya Kasamwa kwa huduma ya kwanza na kisha kuhamishiwa hospitalini kwa matibabu zaidi.

Makore ambaye alikuwa amesafiri kikazi kwenda mkoani Geita, alifikwa na umauti huo majira ya saa mbili usiku katika Kituo cha Afya cha Kasamwa alikopelekwa kwa ajili ya matibabu ya dharura.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC), Edwin Soko, alisema wamesikitishwa kumpoteza mwanachama wao ambaye mwili wake umehamishiwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Geita ukisubiri taratibu nyingine.

Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya The Guardian Limited, Emmanuel Matondo, alisema Makore alikuwa mfanyakazi anayechapa kazi na kampuni ilimwamini na kumkabidhi Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kuisimamia kuhakikisha maudhui muhimu kwa Watanzania yanapatikana.

"Enzi za uhai wake aliishi na wafanyakazi wenzake vizuri, alikuwa na upendo na moyo wa kujituma, kampuni imepoteza mtu muhimu.

"Tunatoa salamu za pole kwa mke wake na watoto, ndugu, jamaa na marafiki. Kwa sasa uongozi wa kampuni unaendelea kuwasiliana na familia yake kwa ajili ya taratibu zote za mazishi ambazo zitatolewa hapo baadae," alisema.

Aidha, alisema kampuni kwa kushirikiana na familia wanafanya taratibu za mwili kutoka Geita kwenda Mwanza huku taratibu zingine za mazishi zikiendelea.

Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe alisema Makore alikuwa miongoni mwa wafanyakazi wachapakazi na tangu ahamishiwe Kanda ya Ziwa amefanya kuwapo kwa uhusiano mzuri baina ya kampuni na vyanzo mbalimbali vya habari pamoja na wateja wanaotangaza na magazeti hayo.

Makore alizaliwa Aprili 20, mwaka 1978. Baada ya kumaliza masomo yake, alijiunga na Kampuni ya The Guardian, Juni 30 mwaka 2015, akiandikia gazeti la Nipashe na Septemba 14 mwaka 2020, alihamishiwa Kanda ya Ziwa.


RAFIKI - SDO

## TENDER NOTICE

## Tender No: RAFIKI-SDO/FY23/TND/003

## Supply of Car Hiring Service

| | | |
|---|---|---|
| Issue date | : | 8th March 2023 |
| Question and Clarification | : | Due by 14th March 2023 |
| Closing Date and Time | : | 21th March 2023, 12:00 PM |
| Date of Solicitation | : | 21th March 2023 |

**Introduction**

RAFIKI-Social Development Organisation (RAFIKI-SDO) is a Non- governmental and Nonprofit making organization working with children, youth, marginalized and vulnerable groups, families and their communities to reach their full potential by advocating their rights and tackling the causes of poverty and injustice. The organization was established in 2005 and registered under NGO Act of 2002, issued with registration number No.00NGO/00006336 to operate in Mainland. Visit us at **www.rafikisdo.or.tz**

The overall object of this notice is to procure car hiring services for staff transport purposes in in Mara,Shinyanga, Geita,Kigoma and Rukwa Region.

**Objective of the tender**

The overall objective of this tender is to procure car hiring services.

| Item No | Item | Item Description | Location |
|---|---|---|---|
| 1 | **Car Hire** | Land Cruiser Hard Top/Prado, 8 seating capacity, Comprehensive insurance cover and well equipped with inevitable car accessories including air conditioning) | Rukwa,Shinyanga,Geita,Mara and Kigoma Regions. |

Interested vendors should download the full terms of reference through **www.rafikisdo.or.tz**

All question and request for qualification should be directed to **procurement@rafikisdo.or.tz** with the subject line request for qualification on supply of car hiring service.

**Eligibility**

To be considered for the award vendor must currently be legally operating in Tanzania and the quotation must include all the following information

- Ability to meet specifications outlined.

**Evaluation criteria**

- Legal eligibility
- Technical capacity and experience.
- Market price.

**Submission instructions**

Interested suppliers must submit the following information to Rafiki-SDO

1. Current company profile
2. Copies of registration certificate,
3. Valid business license,
4. VAT registration certificate (if applicable)
5. Copy of TIN certificates
6. Current Tax clearance
7. Evidence of similar assignments, and at least two (2) names and addresses of client served.

Vendors who wish to apply for this tender should send their proposal in sealed envelopes to Rafiki-SDO Shinyanga Office not later than **21th March 2023, 12:00 PM**

All sealed envelope need to be marked as **"Tender for Car Hire Services"**

**Office address:**

The tender committee Rafiki-SDO
Mbuyuni street,Ndembezi ward.
P.O Box 2078, Shinyanga.
Rafiki-SDO will open all bids on 21th March 2023 at 12:30 PM in presence of bidder's representative who choose to attend.

Quotes must be in Tanzanian shillings and include VAT separately if applicable:

Proposal submitted through email will not be considered

Quotation received after the time or at different address may not be accepted.

# Chongolo aagiza chakula cha msaada

**Na Augusta Njoji,**
SIMANJIRO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kupeleka chakula cha bei nafuu kwenye kata za wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara zinazokabiliwa na njaa kutokana na ukame wa miaka mitatu mfululizo.

Aidha, ameagiza kuondolewa kwa utaratibu wa sasa wa kuwachangisha fedha wananchi ndipo wapelekewe chakula hicho badala yake wapeleke ili wananchi wanunue.

Chongolo alitoa maagizo hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi katika mkutano wa shina namba 26 kwenye kijiji cha Naisinyai wilayani hapa.

Alisema amelibeba suala hilo na kuagiza NFRA kupeleka chakula bila masharti ya kuwataka wananchi kuchangia kwanza na yawekwe kwenye maeneo ambayo wananchi watachukua kwa utaratibu utakaowekwa.

"Wananchi wanataka chakula mimi nitakachokusaidia nitazungumza na hao wanaofungia kwenye maghala wakilete hapa bila masharti ya kwanza wananchi kuchanga fedha. Wasipate tabu mtu aje na fedha yake achukue chakula aondoke," alisema. Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alimwomba Katibu Mkuu huyo kuelekeza serikali kuweka utaratibu rahisi wa uuzaji wa chakula cha bei nafuu tofauti na sasa fedha zinakusanywa kwanza kabla ya kupelekwa chakula.

Alisema ni vyema chakula hicho kikawekwa kwa watendaji wa kata kama vituo vya kuuzia ili wananchi waende na fedha zao kununua.

"Kilichopo ni urasimu na utaratibu uliowekwa ambao ni mgumu unaotaka fedha kwanza zichangwe halafu ndipo watu wachukue fedha hatimaye chakula kiletwe. Katibu Mkuu ukileta chakula kwa watendaji siku mbili watu watakopana fedha na kuchukua mahindi. Tunaomba elekeza serikali iweke utaratibu rahisi badala ya kuchanga fedha na kukaa kusubiri chakula," alisema.

Akizungumzia kuhusu mawasiliano, Mbunge huyo amesema eneo la Meshie na Lengasit na kumuomba Chongolo kuingilia kati kuwasiliana na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ili afikishe mawasiliano hayo.

Awali, Mwenyekiti wa Shina la Naisinyai, Toima Makisen, alisema eneo hilo ndipo yanatoka madini ya Tanzanite kwenye kijiji cha Naisinyai lakini wawekezaji hawakithamini kijiji husika isipokuwa kampuni za Laizer Bilionea na Tanzanite One ambayo awali ilikuwa ikimilikiwa na raia wa kigeni.

"Hawa ndio wameweka michango kwenye kijiji hiki tunatambua Wizara ya Madini ndio wenye mamlaka ya kutoa leseni lakini hutakiwa kuripoti kwa kijiji kinachotoa ardhi ili kinachopatikana kichangie maendeleo ya kijiji.

"Pia geti la kuingilia Mererani limesogezwa mbali na kusababisha kina mama wa kimasai kupata adha na kukosa muda wa kutosha kufanya kazi," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah (wa pili kulia), akijaza mafuta kwenye bajaji ya mwenye ulemavu Sophia Abdallah mkazi wa Mbagala Maji Matitu, wakati kampuni hiyo ilipotoa zawadi ya mafuta na mitungi ya gesi ya kilo sita kwa wanawake wenye ulemavu wanaojihusisha na utoaji huduma ya kusafirisha abiria kwa kutumia chombo hicho, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, katika kituo cha Puma cha Upanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Miili waliokufa katika ajali yaagwa

**Na Neema Hussein,**
MPANDA

MIILI tisa ya watu waliofariki dunia katika ajali ya basi la Komba's katika Mlima Nkondwe, wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, imeagwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda.

Akitoa taarifa mbele ya waombolezaji wakati wa kuaga miili hiyo juzi, Katibu Tawala Mkoa wa Katavi, Hassan Rugwa, alisema miongoni mwa watu hao walioifariki dunia, wawili ni wa kutoka familia moja huku mmoja akiwa mjamzito wa takriban wiki 20.

Rugwa alisema miili saba Kati ya 9 imetambuliwa huku miili miwili ikiwa bado haijatambuliwa na kwamba licha ya kuagwa, imerejeshwa katika chumba cha maiti kwa ajili ya kusubiri kutambuliwa na ndugu.

Alisema majeruhi 39 wanaendelea na matibabu huku kati yao, wanne wamesafirishwa kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, jinini Mwanza kwa matibabu zaidi.

Katibu Tawala huyo alisema chanzo cha ajali kinasadikiwa kuwa ni kufeli kwa breki kwa basi hilo kulikosababisha kuacha njia katoka mteremko mkali wa mlima Nkondwe na kutumbukia kwenye korongo lililo umbali wa takribani mita 75 kutoka usawa wa barabara.

Pamoja na kutajwa kwa chanzo hicho, alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo halisi.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, ambaye aliongoza wananchi na viongozi kuaga miili hiyo, aliwataka wasafirishaji na madereva wa abiria ndani ya mkoa wa Katavi, kuendelea kuwa makini wanapokuwa barabarani ikiwa ni pamoja na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Pia alilielekeza Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha ukaguzi, usimamizi, udhibiti na ufuatiliaji wa vyombo mbalimbali vinavyobeba abiria unafanyika kwa umakini zaidi ili kudhibiti ajali za barabarani. "Kama nilivyoelezwa kwamba ajali ile ilitokana na dereva kushindwa kulimudu gari, sasa kwa kuwa uchunguzi unaendelea ili kubaini kwa nini hakuweza kulimudu gari, itakapobainika hatua stahiki tutazichukua kikamilifu," alisema Mrindoko. Habari zaidi zinasema miongoni mwa watu waliopoteza maisha katika ajali hiyo ni Katibu wa Wazazi wa Chama Cha Mapindizi (CCM) Kata ya Makanyagio, Anisiata Kapandila.

## Sekta binafsi yatakiwa kuwapa nafasi wanawake

**Na Romana Mallya**

SEKTA binafsi imeombwa kuwapa nafasi wanawake katika masuala ya teknolojia na ubunifu, ili waweze kutengeneza vifaa ambavyo vitatatua matatizo ndani ya jamii.

Ofisa wa Mpango wa Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kutoka UN Women Tanzania, Lilian Mwamdanga, aliyesema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyokutanisha wadau wa kitaifa na kimataifa.

Maadhimisho hayo yamebebwa na kaulimbiu: 'Ring the Bell for Gender Equality' ikimaanisha Piga Kengele kwa Usawa wa Kijinsia.

"Sekta binafsi ni wadau wakubwa wa maendeleo, wanatengeneza ajira na pia kuwasaidia wanawake kutengeneza vifaa vya teknolojia mbalimbali," alisema.

Pia, aliiomba sekta binafsi kuja na sera mpya ambayo itahusiana na masuala ya teknolojia na kutoa elimu ya mila zinazowakandamiza wanawake wasiweze kutimiza malengo yao.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTRADE), Latifa Hamis, akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema kaulimbiu ya mwaka huu imelenga kukuza usawa wa kijinsia.

"Kwa mfano, uvumbuzi na teknolojia zinaweza kuchangia kufikia lengo hili kwa kuziba pengo la kidijitali," alisema.

Alisema wanaweza kuwasaidia wanawake kupata ujuzi na maarifa wanaohitaji ili kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali.

Mshauri Mwandamizi Masuala ya Jinsia, Afya na Maendeleo, kutoka Kamati ya Rais ya Ushauri kwenye Masuala ya Usawa wa Jinsia (GEF), Grace Munisi, alisema Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ina umuhimu mkubwa kwa wanawake kwa sababu akiwa sehemu yoyote ana uwezo kuitumia kujipatia kipato.

"Tunatakiwa kuwekeza katika TEHAMA ili kupunguza tatizo la uhaba wa ajira kwa wanawake na wasichana," alisema.

Mkutano huo umeandaliwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa kushirikiana na Shirika la UN Global Compact Network Tanzania, UN Women Tanzania, UN Women Sustainable Stock Exchanges Initiative (SSE), United Nations Tanzania, and International Finance Corporate (IFC) kwa ufadhili wa Shirika la TTCL Pesa na benki ya Stanbic.

TANGAZO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

## Kusudio la Kufuta Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara Wasio na Sifa za Kuendelea Kusajiliwa katika VAT

**Dar es Salaam, 01 Machi, 2023:**

Kwa mujibu wa **Kifungu 28** na **29 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 (Rekebisho la Mwaka 2019),** wafanyabiashara waliotimiza vigezo vya kusajiliwa katika Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), wanatakiwa kuomba usajili huo kwa Kamishna Mkuu. Moja ya vigezo vya kusajiliwa katika VAT ni kuwa na mauzo kwa mwaka, yanayozidi kiwango cha chini kilichowekwa na **Kanuni ya 14 ya Kanuni za VAT za mwaka 2015** cha **Shilingi Milioni Mia Moja.**

Tathmini iliyofanyika kupitia kumbukumbu zetu za usajili wa VAT imebainisha kuwa, baadhi ya walipakodi waliosajiliwa katika VAT, wamepoteza sifa za kuendelea kuwa katika usajili ikiwa ni pamoja na biashara zao kutofikisha mauzo ya milioni mia moja kwa mwaka. Ili kuimarisha usimamizi mzuri katika VAT, Kamishna Mkuu anakusudia kutumia mamlaka aliyokasimiwa chini ya **Kifungu cha 41 cha Sheria ya VAT**, kuwafutia usajili walipakodi wote wenye mauzo chini ya kiwango tajwa, pamoja na wale waliopoteza sifa zilizoainishwa chini ya **Kifungu cha 29 cha Sheria ya VAT. Hata hivyo, kusudio hili halilengi kumuondolea mlipakodi wajibu wake wa kulipa kodi au kuwasilisha ritani za kodi za kipindi cha nyuma kwa walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT.**

Kutokana na ufafanuzi huu, tunawajulisha kuwa **orodha kamili ya majina ya walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT imewekwa kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz).** Mlipakodi yeyote mwenye pingamizi juu ya maamuzi ya Kamishna Mkuu, anatakiwa kuwasilisha pingamizi lake, akielezea sababu za kwanini asifutiwe usajiliwa VAT. Pingamizi ziwasilishwe katika **Ofisi za TRA kwa Meneja wa Mkoa husika** na **ziwasilishwe ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya notisi hii.** Baada ya siku 30 zilizowekwa kupita, Mamlaka itaendelea na zoezi la kufuta usajili wa VAT.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo

| | |
|---|---|
| **Tovuti:** | www.tra.go.tz |
| **Namba ya Bure:** | 0800 750 075 au 0800 780 078 |
| **WhatsApp:** | 0744 23 33 33 |
| **Barua Pepe:** | huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Kidatah

A.J. Kidata

**Kamishna Mkuu**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila siku ajali zinamaliza nguvukazi ya taifa

**MATUKIO** ya ajali zinazotokea kila siku nchini na kugharimu maisha ya Watanzania hayana budi kudhibitiwa ili taifa lisiendelee kupoteza nguvukazi.

Katika kipindi cha kuanzia mwisho wa mwaka 2022 hadi mwaka huu, matukio ya ajali yameendelea kutokea na watu wanaopoteza maisha ni wengi.

Ajali nyingi chanzo chake ni mwendo kasi na madereva kutozingatia alama za barabarani. Juzi kumeripotiwa ajali iliyotokea mkoani Katavi wilayani Tanganyika na kuondoka na maisha ya watu tisa huku wengine 30 wakiachwa na majeraha makubwa.

Uchungu wa kuondokewa na watu hao haujatoka mioyoni mwa ndugu, ajali nyingine inatokea Katavi na kuua watu saba miongoni mwao akiwa Mwakilishi wa Nipashe mkoani Mwanza, Richard Makore. Ni pigo kubwa sana kwa familia ya The Guardian kumpoteza Richard Makore, ambaye mpaka siku anayopata ajali alikuwa akitaniana na waandishi wenzake kwenye grupu lao la kupeana habari kimtandao. Kwa wafanyakazi wa The Guardian Limited haikuwa rahisi kuamini baada ya kupata taarifa ya kutokea kwa ajali hiyo na yeye akiripotiwa kuwa mmoja wa abiria waliokuwa kwenye basi hilo lililopata ajali.

Wakati juhudi za kufuatilia zikiendelea waandishi wanzake walikuwa wakimwomba Mungu Makore asipatwe na jambo baya, lakini baada ya kutambuliwa majeruhi waliokuwamo kwenye ajali hiyo na yeye jina lake kukosekana kwenye orodha hiyo, imani ya wengi ilianza kupotea kuwa Makore atakuwa hai.

Juhudi za kufuatilia Hospitali ya Bugando, mkoani Mwanza na Geita zilianza kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti na hapo ndipo uhakika ulipopatikana kuwa Makore hayupo duniani akiwa ni mmoja waliofariki kwenye ajali hiyo.

Makore alikuwa bado kijana aliyekuwa tegemeo kubwa si kwa familia yake tu, bali hata kwa kampuni ya The Guardian aliyokuwa akifanyia kazi kutokana na uwakilishi wake mzuri kwa kushirikiana na timu yake ya Kanda ya Ziwa katika kupasha habari za kanda hiyo.

Makore pamoja na watu wengine waliopoteza maisha kwenye ajali hiyo wameacha vilio na uchungu mkubwa kwenye familia zao. Watoto walikuwa wakiwategemea, wazazi waliokuwa wakiwategemea, wake wao walikuwa wakiwategemea na waume zao walikuwa wakiwategemea.

Vifo havipangwi, lakini vifo vya ajali vinaweza kuzuilika kama madereva wanaoendesha vyombo vya moto watakuwa makini kwa kuhakikisha wanafuata sheria za usalama barabarani na magari wanayoendesha yanakuwa salama kabla ya kuanza safari. Madereva pia wawe makini kwa kutoruhusu kujaza abiria kupita kiasi kutokana madai ya makondakta na madereva magari ya mkoani kuchukua abiria wa ziada ili pesa hiyo iingie mikononi mwao na ile halali ya siti ndio anayopelekewa mmiliki. Askari wa Usalama Barabarani wasichoke kutimiza wajibu wao kwa kukagua magari hayo yanapokuwa njiani ili kuepuka ajali hizo zinazojitokeza mara kwa mara kwa sababu ya uzembe wa madereva wa kutozingatia usalama wa abiria na barabara wanazopita.

Abiria pia wanapoona dereva anaendesha mwendo unao hatarisha maisha yao, watoe ripoti kwa kuwapigia polisi wa usalama barabarani kudhibiti hatari isitokee na kuleta madhara makubwa ambayo yanashuhudiwa kutokea kila kukicha.

Kwa pamoja abiria wakishirikiana kudhibiti madereva wasiofuata sheria za usalama barabarani, ajali zitaepukwa na kunusuru maisha ya Watanzania wanaotegemewa kuleta maendeleo ya nchi yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Pilly Kigome

# Kinamama siku yetu tumeiona, sasa ni kusonga dira mabadiliko chanya

**KILA** inapofika Machi 8 ya mwaka, siku kama ya jana, wanawake wote duniani tunasherehekea siku maalum kwa ajili kutambua hadhi na nafasi yetu katika jamii, tukiendeleza mshikamano wa dhati baina yetu.

Ni raha ya aina yake, pale iliponogeshwa jana na mkuu wa nchi, Dk. Samia Suluhu Hassan, naye akatia mguu kuweka historia kuwa mgeni rasmi katika kikao cha Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), kupaka gundi na kuweka kifuli la mshikamano zaidi.

Wapo wanayoitumia siku hiyo kwa kufurahi kutembea sehemu mbalimbali, wapo wanaotumia siku hiyo kutembeleana kama zilivyo sikukuu zingine za kidini au za kiserikali.

Pia wapo wanayoitumia sikukuu hii kwa kubadilishana mawazo kwa mikusanyiko mbalimbali maalum ya wanawake kwa kuongezeana ama maarifa au uwezo unaoimarisha, siku hiyo ikamilike.

Hivyo, tukiwa kama wanawake hasa naomba nizungumze na wanawake wa Tanzania, ili kuweza kuleta tija na kuweza kuleta mabadiliko katika jamii yetu.

Tunaposema mwanamke, ni jina kubwa sana katika jamii yetu ya Kitanzania na duniani kote kwa ujumla, hakuna asiyejua umuhimu wa mwanamke katika maisha yetu ya kila siku.

Hivyo, tunatakiwa tujitathmini tujipambanue na kujitambua pia umuhimu wetu hasa katika jamii yetu iliyotuzunguka, maana sisi wanawake ni kioo cha jamii na cha familia pia.

Inashangaza kuona kwamba, mwanamke anakuwa ni mtu wa ovyo katika jamii yetu hii ya Kitanzania, kwani ni jambo la kusikitisha. Hiyo ni kwa sababu mwanamke ni mlezi na ndiye anastahili awe mfano, kwani ameumbwa kwa kuujaza ulimwengu wake.

Ninaona utata pale tunapoendelea kuona wanawake wakitupa watoto mitaroni. Vilevile inashangaza kuona wanawake hao wakiwa wanafanya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia majumbani, kwa watoto na wanaume.

Ni jambo gumu kwao, pale kuna hali ya wanawake wakiendelea kishiriki vitendo vinavyovunja amani katika jamii ya Kitanzania.

Mimi naona, tukiwa katika kilele hiki la kutabasamu na siku yetu katika nafasi ya mama zaidi, nisiyechukizwa na vitendo viovu vinavyofanywa na wanawake, hata kuvunja heshima ya nafsi yake.

Ninawaomba sana wanawake wenzangu, kwanza tubadilike katika mwenendo na tabia kwa ujumla, ili jamii yote ione uhalisia wa mwanamke kubaki kuwa mtu muhimu kuliko yeyote duniani. Wito wangu sasa ni tulete mabadiliko katika jamii yetu na tuwe mfano wa kuigwa, pia na tuwe mfano wa kuigwa na si kwenda kinyume na kuudhi viumbe wengine duniani.

Licha ya wanawake kuendelea kujitahidi kutetea haki zetu kila kukicha, pia tuchukue nafasi yetu katika kutetea haki za wenzetu na tuachane na yote tusiyopenda kufanyiwa, hata kuwachukiza wengine.

Kumekuwapo wimbi la wanawake wanaopenda kutumia vibaya kasi ya teknolojia ikikua duiniani, kwani wamekuwa wakitumia mwanya huo kuharibu na kubomoa familia zao bila ya kujitambua.

Nasema hivi, kwa sababu teknolojia nayo imekuwa katika nafasi ya kubomoa utamaduni na mila zetu, kwa matumizi mbalimbali ya nyenzo, zikiwamo televisheni na simu, ambazo zimekuwa zikikua kwa kasi sana na kujikuta sisi wanawake tunabomoa maadili kwa watoto wetu bila ya kutambua au kujitambua.

Simu ni mfano mojawapo wa nyenzo hatari, kwani tukiwa tukiwaachia watoto watumishi ikiwa ni sehemu ya mapenzi kwa watoto hao, kumbe kinyume chake, tunabomoa kwa kuibua mmomonyoko wa maadili, bila ya kutambua.

Napenda kuipongeza serikali na wadau wengine kwa ujumla ambao tayari wamejitokeza na wanaoendelea kujitokeza ili kuweza kuwasaidia wanawake waweze kujikwamua kiuchumi, ili kuwawezesha kuleta tija katika jamii yetu.

Serikali yetu ya Tanzania inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imekuwa ni ya mfano katika kupigania maslahi ya wanawake na kuhakikisha wanawake wanajiweza kujikwamua kiuchumi.

Hivyo, tukiwa katika nafasi yetu ya uanawake, serikali imekuwa ikitupigania na imeweza kutoa fedha kwa ajili yetu, hivyo tutumie vizuri fursa hii adhimu ya kuona serikali inatujali lengo ni kunyanyua wanawake kuwa imara kiuchumi.

## HABARI PICHANI

# WAFANYAKAZI WANAWAKE WA KAMPUNI YA THE GUARDIAN LTD (TGL) WAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI




Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga, akiwa pamoja na wafanyakazi wanawake wa kampuni hiyo. **PICHA: JOHN BADI**



Mkurugenzi wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Joyce Luhanga (wa tano kulia), akiwaongoza wafanyakazi wanawake wa TGL kusimama dakika moja kwa ajili ya kumkumbuka mwandishi wa habari wa gazeti la Nipashe, marehemu Richard Makore aliyefariki kwa ajali ya gari mkoani Geita juzi, kabla ya kuanza halfa fupi ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Mikocheni Dar es Salaam jana. Kulia ni Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe. **PICHA: JOHN BADI**




Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), akiwaongoza baadhi ya wafanyakazi wanawake wa TGL, kuonyesha ishara ya usawa wa kijinsia kabla ya kukabidhi msaada wa vitu mbalimbali katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga, akikata keki kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JOHN BADI**



Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, Ofisa Utawala wa TGL, Rehema Shedrack (wa pili kulia) na Mhariri wa Habari Nipashe, Salome Kitomary (wa tano kulia), wakiungana na wafanyakazi wanawake kupiga 'cheers' huku wakiwa na furaha ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JOHN BADI**

# CHADEMA kuanza operesheni mpya

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza kuja na operesheni mpya ya kitaifa mwishoni mwa Machi itakayokipeleka chama hicho kila mkoa, jimbo, kata, kijiji na mtaa, kwa mwaka mzima.

Lengo ni kujisogeza karibu na wananchi baada ya kuondolewa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa lililodumu kwa zaidi ya miaka saba.

Rais Samia Suluhu Hassan, aliondoa zuio hilo Januari 3, mwaka huu, wakati akizungumza na viongozi wa kitaifa wa vyama vya siasa nchini, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia ujio wa operesheni hiyo na uzinduzi wake, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alisema Kamati Kuu ya chama hicho iliyokutana Machi 4, mwaka huu, ilifanya tathmini ya mambo mbalimbali, lakini yapo waliyokubaliana ambayo lazima yafanyike. "Jambo moja, ambalo tulikubaliana ni kwamba kama chama, tunapaswa kwenda kwenye operesheni maalum ya chama.

"Kwamba kama chama, tunapaswa kwenda kwenye operesheni maalum ya chama ambayo sitaizindua leo na wala sitaeleza jina lake leo, lakini itoshe kuwaambia kwamba tutazindua operesheni maalum ya chama.

"Tumepanga tutaanzia Mkoa wa Kigoma, mwisho wa mwezi huu na tutaendelea Katavi na Tabora.

"Tutakwenda Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara na tutamaliza awamu hiyo katika Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi na kisha tutaendelea kanda nyingine kwa ratiba ambayo baadaye itawekwa wazi na chama."

Hiyo itakuwa ni operesheni ya saba ya CHADEMA, baada ya kutanguliwa na Operesheni Kata Funua, Operesheni Chadema ni Tawi, Operesheni Sangara, Operesheni Chadema ni msingi, Vuguvugu la Mabadiliko (M4C) na Operesheni Mshike Mshike. Kabla ya Mbowe, kudokeza ujio wa operesheni mpya maalum, mwezi uliopita kulifanya mikutano ya kisiasa katika Kanda ya Nyasa inayojumuisha mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa na Njombe.




Mkuu wa Matawi ya Benki ya Exim, Agnes Kaganda (wa pili kulia), akizungumza wakati akitambulisha huduma mpya ya akaunti maalum kwa ajili ya wanawake ijulikanayo kwa jina la 'Supa Woman' ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Matawi wa Kanda wa benki hiyo, Elizabeth Mayengo (kulia), Mkuu wa Bidhaa za Rejareja na Uhakika wa Mapato, Mtenya Cheya (wa pili kushoto) na Meneja Msaidizi Masoko na Mawasiliano, Mariam Mwapinga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kasi matukio ukatili watoto yazidi

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Kituo cha Polisi cha Songwe na Ofisa Polisi Kata ya Bonde la Songwe, mkoani Mbeya, Inspekta Dominic Mawala, amesema taarifa zinazohusu watoto kuingiliwa kinyume cha maumbile zimekuwa zikipokewa mara kadhaa kituoni hapo.

Amesema pamoja na taarifa kupokewa ikiwamo na baadhi ya watuhumiwa kufikishwa kituoni hapo na wananchi, ushahidi hukosekana kwa kuwa ushirikiano na elimu kuhusu matukio hayo bado ni duni.

Inspekta Mawala aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi katika Kata ya Bonde la Songwe, ikiwa ni maadhimisho ya kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani yanayofanyika leo.

"Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 namba 21, inatoa ulinzi na haki kwa mtoto kupata elimu, burudani. Tumepokea kesi nyingi kwa mfano watoto kuingiliwa kinyume na maumbile na watu wazima na madhara yake wanapata maambukizi VVU na magonjwa ya zinaa.

"Tunatoa elimu mwamko unaongezeka na vyombo vinatoa haki na watenda makosa wanaadhibiwa. Wananchi wanaokumbana na madhila hayo washiriki na tunapowaita mbele ya mahakama kuthibitisha, wawe wanafika," alisema.

Alisema changamoto iliyopo ni uelewa mdogo kuhusu haki na sheria, wananchi baadhi wakidhani polisi jukumu lao ni kutoa adhabu kwa watuhumiwa wa matukio hayo, akisema hilo linaihusu mahakama baada ya kujiridhisha.

Devarine Mgoda, Ofisa Maendeleo ya Jamii anayeshughulikia masuala ya Wanawake na Watoto, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema kata moja huchaguliwa kuadhimisha siku hiyo, ikipendekezwa Bonde la Songwe, mwaka huu.

Alisema maadhimisho hayo huenda sambamba na mafunzo wiki moja kabla ya kilele, na kwamba wamebaini elimu inahitajika kuhusu masuala ya wanawake na watoto, ikiwamo kuepukana na ukatili.

Christopher Sawanga, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Songwe-Viwandani, alisema maadhimisho hayo yakiadhimishwa kwenye eneo lake kimkoa, yanaongeza kasi ya wananchi kuripoti matukio ya ukatili yanayotokea eneo hilo.

"Huwa tunashirikiana na maofisa kutoa elimu na kupokea taarifa. Tunashirikiana na taasisi za kiraia kuhusu masuala ya kijamii na vilevile viongozi wenzangu wa vitongoji waisambaze elimu hii kwenye maeneo yao," alisema Sawanga.

Thobias Ndawi, mkazi wa kijiji cha Idiga, alisema kwamba wanaume pia wamehamasika kushiriki maandalizi ya siku ya wanawake, ili kupata elimu kutokana na mafunzo mbalimbali waliyopewa.

"Mwanaume anakufa mapema kutokana na msongo wa mawazo, kumbe anapigwa na mkewe lakini anakaa kimya, lakini ukijichanganya kama hivi unapata elimu, unabaini je, upo wapi.

"Kinamama hawa pia kushirikiana nao huwa ni msaada mkubwa, wanaishika familia, na pia katika mirathi tuweke wazi ili wasije wakadhulumiwa baadaye," alisema Ndawi.

Tabitha Bugali, Mkurugenzi Mtendaji wa Sauti ya Mama Afrika Foundation (SAMAFO), alisema wametoa mafunzo kwa Kijiji cha Viwandani, kata ya Bonde la Songwe, kuelezea aina, viashiria vya ukatili kwa kushirikiana na watoa msaada wa kisheria na dawati la Jeshi la Polisi.

Alisema pia maofisa ustawi na maendeleo ya jamii, wameshirikishwa ili kuelezea masuala hayo huku akisema kaulimbiu ya mwaka huu ni "Teknolojia na Ubunifu kwa Matarajio ya Kuwapata Wabunifu ambao hawakukwamishwa Nyuma na Vitendo vya Ukatili."

## Wafundishwa ujasiriamali kukabili ugumu wa maisha

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Misaada la Kimataifa la Kulea Childcare Villages limewasaidia Watanzania 1,500 wengi wakiwa wanawake wanaolea watoto wenyewe na kuishi mazingira magumu, kunufaika na elimu ya ujasiriamali na mradi wa Maisha Matters.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Mkurugenzi Mtendaji wa Childcare Villagers nchini, Paul Magaya, alisema mbali na elimu pia wanahudumia watoto yatima ambao wazazi wao walifariki wakati au baada ya kujifungua.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya wanawake nchini wametelekezwa na wanalea watoto wao katika mazingira magumu na kwamba wanashirikiana na serikali na hospitali za rufani kuwapata na kuwapatia mtaji na elimu ya kuanzisha biashara kwa mwaka mmoja ili iwasaidie kujikwamua na kumudu gharama za maisha.

"Watoto hawa tunawapata kupitia rufani maalum na Wizara ya Mambo ya Ndani imetupa kibali cha kufanya kazi na hospitali tano za mkoa wa Dar es Salaam zikiwamo ya Amana, Temeke, Kigamboni, Mwananyamala na Muhimbili, pia tuna mpango wa kuomba kibali tufikie hospitali za kata na wilaya," alisema Magaya.

Aidha, alibainisha kuwa wapo wanawake na watoto ambao pia wanaingia katika mradi huo kupitia maofisa wa ustawi wa jamii na maendeleo wa kata na wengine ambao wamepewa mamlaka ya kutoa barua za rufani na idhini.

Pia, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, na watendaji wa ngazi mbalimbali za serikali kwa kuwapatia ushirikiano kwa lengo la kusaidia watoto, wanawake na wanaume waliopoteza wake zao na kuachiwa jukumu la kulea watoto.

Kwa mujibu wa Magaya, kila Jumanne wazazi au walezi wanapeleka watoto kituoni hapo kwa ajili ya kupimwa na kuangaliwa maendeleo yao ya ukuaji, pamoja na kuangalia viashiria vya unyanyasaji wa kijinsia.

Tausi Salimu, mwenye watoto mapacha watatu na mnufaika wa mradi huo, alisema awali alitelekezwa na baba wa watoto wake kabla hajajifungua na ilimsababisha kuishi maisha ya shida bila kujua anawaleaje watoto hao.

"Nashukuru Mungu baada ya kuchukuliwa na shirika hili lilinisaidia kuwaangalia watoto wangu katika malezi, walinipatia mtaji usiokuwa na riba na elimu ya namna ya kuanzisha biashara dogo, ambayo imenisaidia kumudu gharama za maisha mpaka sasa naendelea vizuri," alisema Tausi.

Ofisa Muuguzi wa shirika hilo na Mratibu wa mradi wa Maisha Matters, Flora Saasita, alisema wamekuwa wakijikita pia kuwapa wanawake elimu ya afya namna ya kujilinda na magonjwa na jinsi ya kuwalea watoto vizuri.

Alisema watu wote wanaowapatia huduma wamepewa rufani kutoka hospitali na baada ya kuwapokea wanaenda kwanza katika makazi yao, ili kuhakikisha hakuna kitu chochote kitakacho kwamisha huduma watakayompatia, pamoja na kujua hali yake ya kimaisha ili wamsaidie kulingana na uhitaji.

"Kuna kinamama walikuja na watoto wakiwa na utapiamlo lakini baada ya kuwapatia huduma sasa hivi wanaenda vizuri, wengine pamoja na kuwapatia lishe, lakini hawaji vizuri kama tunavyotarajia, tunajitahidi kuwapa elimu ya usafi na kila mtoto analipiwa bima ya afya ya mwaka mmoja ili kuhakikisha wanakua vizuri," alisema Flora.





# Wakazi vijiji 12 wamwangukia Chongolo mgogoro wa mipaka

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANANCHI kutoka vijiji 12 vya Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Manyara na Tarangire, wamemwomba Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, kuwasilisha kilio chao serikalini kuhusu suluhu ya mpaka kati yao na hifadhi hizo.

Pia wamemwomba kufikisha kilio chao cha wanyamapori kuingia katika makazi yao na kufanya uharibifu wa mali na maisha ya wananchi.

Diwani wa Kata ya Magara katika Halmashauri hiyo, Jacob Fundi na Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo (CCM), wametoa maombi hayo juzi baada ya Katibu Mkuu huyo kusimama na kuzungumza na wananchi wa Magara, wakati akianza ziara yake wilayani Babati.

Akizungumzia mgogoro wa mpaka kati ya hifadhi hizo na vijiji hivyo, Sillo alisema wananchi wana mgogoro wa mpaka baina yao na hifadhi hizo na haijawahi kupatiwa ufumbuzi.

Aidha, alimwomba Chongolo kuwasaidia kufikisha kilio chao kwa serikali, ili wanyamapori wanaoingia vijijini humo kutoka kwenye hifadhi hizo na kuharibu mazao yao, walipwe fidia inayolingana na uharibifu uliofanywa.

Akijibu maombi hayo, Chongolo alisema atazungumza na Waziri wa Maliasili na Utalii ili aje kukaa na wananchi hao, kuwasikiliza na wabainishe alama za mipaka ili kumaliza mgogoro uliopo.

Chongolo alisema: "Ninakwenda kuzungumza na waziri husika aje hapa azungumze nanyi, awaonyeshe alama za mipaka halisi, lakini hili la wanyamapori wanapokuja kwa wananchi na kuleta uharibifu, lazima mamlaka husika iwalipe fidia, kulingana na uharibifu uliofanywa".

# Wanawake watakiwa kutafakari vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa wanaume

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI wa Shirika la Maendeleo la TUSINGE CDO, Aginatha Rutazaa, amewapa somo wanawake akiwataka kuitumia Siku ya Wanawake Duniani kutafakari kuhusu vitendo vya ukatili vinavyofanyika dhidi ya wanaume kwenye ndoa.

Alisema kwa kuwa katika karne hii jamii imekimbilia suala la kukuza usawa wa kijinsia katika kundi la kinamama, wasichana na watu wenye ulemavu, wakisahau vitendo vya wanaume kunyanyaswa na wenzi wao.

"Tunapoherehekea siku yetu kinamama tujiulize, yule mwanaume wako nyumbani ni kwa namna gani umemsaidia baba kujisikia ni sehemu ya huyu mama kudumisha ndoa yako, ili baba akiingia nyumbani awe anaingia na ujasiri kama baba, kama babu wa wajukuu, baba wa watoto na mume wa mke aliyeko kule ndani.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yanaongozwa na kauli mbiu isemayo, 'Ubunifu na mabadiliko ya teknolojia, chanzo katika kuleta usawa wa kijinsia'.

"Ni vizuri tutumie muda huu kujitafakari. Kwamba sisi kama kinababa tumekaa kwenye nafasi zetu, tumesimama vizuri? Tumevaa viatu vyetu kwenye ndoa sawa sawa! Tumevaa viatu vyetu kama mama ndani ya familia, ambayo inalea watoto wako sawa sawa.

Zaidi aliongeza, "Tumetenga muda wetu vizuri wa kulea? Tunajua mama ndiye mlezi mkuu wa familia. Baba anatafuta, mama anakuwa analea sana, kwa sababu kwanza tuna fursa ya kuwa na hiyo mifuko kwenye matumbo yetu ya kubeba watoto, ni baraka kubwa Mungu ametupa. Tumewabeba tumboni miezi tisa, tunatoka tunakaa nao, tunawanyonyesha na tunawalea. Mpaka mama atoke aende barabarani ni zaidi ya miaka miwili."


Aidha, baadhi ya wadau wa TUSONGE CDO, akiwamo Vaileth John, alisema teknolojia ni nzuri, lakini pale ambapo inatumika vibaya huwa inaleta madhara hasa katika masuala ya ukatili wa kingono.

"Unakuta wanawake na wasichana ama watoto wanakuwa wanadhalilishwa mitandaoni kwa kuitumia teknolojia vibaya. Unakuta wanawake wanatuma picha za utupu zinatupwa mitandaoni, huo ni udhalilishaji. Unakuta mahusiano yao ama maisha yao ya usiri yanatumwa mitandaoni, huo ni udhalilishaji," alisema.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake na Wasichana Wenye Ulemavu, Mkoa wa Kilimanjaro, ambaye ni mnufaika wa TUSONGE CDO, Linda Macha, alisema watu wenye ulemavu na masuala ya kidijitali, kuweka bando kwenye simu ni ngumu kwao kwa sababu hawana pesa ya kununua mahitaji yake na kupata taarifa kupitia kidijitali.

Alisisitiza kuwa mambo ya dijitali yanataka kila saa uwe mtandaoni na kumwelimisha mtu mwenye ulemavu pia ni changamoto inahitaji hatua kwa hatua.

Ofisa Miradi wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima, Mkoa wa Kilimanjaro (MVIWAKI), Stefano Msuya, alisema wakati yanafanya maadhimisho haya wamegundua kinababa nao wanapitia ukatili wa kingono.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogoro (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Isidori Msaki (kulia kwake), wakikabidhi mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. milioni 790 kwa wawakilishi wa vikundi 16 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama mikopo ya mapato ya asilimia 10 ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanawake vyombo vya ulinzi watoa msaada kwa wajane

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANAWAKE kutoka vyombo vya ulinzi na usalama mkoani Manyara, wametoa msaada kwa familia mbili za wajane wilayani Babati na Hanang', kwa kuzipatia vyakula na pikipiki.

Msaada huo umetolewa kupitia Mtandao wa Polisi Wanawake (TFNET) ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Wajane waliopatiwa msaada huo ni Zaituni Haji, kutoka Kitongoji cha Walangi B kilichoko Wilaya ya Babati na Paskalina Gidad wa Kijiji cha Ming'enyi wilayani Hanang'.

Akizungumza wakati wa kukabidhi misaada hiyo, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Manyara, Georgina Mtagi, alisema wamekabidhi pikipiki moja kwa kila familia hizo, ili wazitumie kuinua kipato cha familia.

Alitaja vitu vingine walivyowasaidia ni magodoro, sabuni, vyakula na nguo ili nao washerehekee siku hiyo kwa furaha.

"Tuliowapatia misaada hii ni familia zinazohitaji msaada na tulizipata kupitia utafiti tuliofanya, kupitia viongozi wa kata na vijiji vyote vya wilaya zote mkoani hapo. Hawa kweli wanastahili,"alisema.

Alisema Zaituni alifiwa na mume wake akiwa hana kiwanja ila alipambana akapata kiwanja na kujenga chumba kimoja.

Mtagi alisema kazi kubwa anayojishughulisha nayo ni ulimaji wa mboga, kwamba watoto wake ndiyo wanauza mitaani ili wapate fedha za kujikimu kimaisha na kwenda shule.

Alisema watoto hao hulazimika kutembeza mboga mtaani na baadaye ndipo wanakwenda shule, hali inayowasababisha wakati mwingine kutokwenda.

Alisema kwa msaada wa pikipiki waliompatia itaondoa tatizo hilo la utoro, kwamba wataanza kupata kipato na kuwahi shule bila kikwazo.

Kuhusu mjane Paskalina, Mtagi alisema watoto wake walikuwa wanalala na mifugo ikiwamo mbuzi na nguruwe kwa sababu ya ugumu wa maisha. Wakizungumza baada ya kupokea msaada huo, mjane Zaitun Haji alishukuru kupewa msaada huo.

Alisema wakati wote alikuwa analala kanisani akiomba Mungu amuinue na sasa amemjibu.

Mjane mwingine Paskalina Gidad alishukuru kwa kupewa msaada wa pikipiki, vyakula, sabuni, mashuka, mablanketi na nguo.

Mkuu wa Wilaya ya Hanan'g, Janeth Mayanja, aliwapongeza wanawake hao kwa kutoa msaada huo na kuwataka kupigania usawa wa kijinsia katika jamii kwa kuwa harakati hizo zinaanza na wao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ming'enyi, Karan Sadan, aliahidi kutoa mabati 40 ili kumjengea nyumba mjane Paskalina.

Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Kamishna Msaidizi wa Polisi, George Katabazi aliwapongeza wanawake hao kwa kuonyesha mfano kwa wengine.

Vikosi vilivyoshiriki katika kutoa msaada huo ni kutoka Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji, Uhamiaji, Hifadhi ya Taifa Tarangire, Taasisi ya Wanyama Pori (TAWIRI), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) pamoja na SUMA JKT.

## Watoto, wanawake 781 wafanyiwa ukatili wa kijinsia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIBU wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Asha Kitandala, amesema watoto na wanawake 781 mkoani Shinyanga wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alitoa takwimu hizo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi kilichopo kata ya Nyihongo-Manispaa ya Kahama.

Alisema kutokana na matukio hayo kesi 234 zinaendelea kusikilizwa mahakamani, 106 wahusika walishinda mashauri, 73 zikishindwa kuendelea mahakamani kwa kukosa ushahidi wa kutosheleza, huku kesi 287 zikiendelea na upelelezi.

Alisema katika matukio ya ukatili wa ubakaji kulikuwa na matukio 192, ulawiti 40 pamoja na mimba za wanafunzi 157 kutoka katika Halmashauri za Shinyanga, Manispaa ya Kahama, Kishapu, Msalala na Halmashauri ya Ushetu.

Kitandala alisema matukio mengi ya ukatili wa kijinsia kwa kiwango kikubwa yanafanywa na wanawake kwenye jamii, huku akiwasihi kubadilika. "Mkoa wetu umendelea kuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia kwa watoto kulingainisha na mikoa mingine kutokana na kuwa na takwimu kubwa na matukio yanayotokea katika halmashauri zetu, hivyo tushirikiane pamoja kutokomeza ukatili huu,"alisema Kitandala.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2020 matukio 812 yaliripotiwa katika vyombo vya sheria, kati ya hayo mashauri 32 yanaendelea kusikilizwa mahakamani, 106 zilishinda, 169 zikishindwa kwa kukosa ushahidi, huku 204 zikiendelea na upelelezi. Mwenyekiti wa UWT, Grace Samweli aliwataka wanawake kuacha tabia ya kuingia kwenye michezo ya kukopeshana fedha, akisema michezo hiyo imekuwa moja ya sababu ya wanawake wengi kuzikimbia familia zao pale wanaposhindwa kufanya marejesho kwa wakati.

Alisema wanawake wamekuwa na tabia ya kukopa viwango vikubwa vya fedha kulinganisha na hali za maisha yao, hali ambayo fedha zinatumika katika matumizi ambayo hayakulengwa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa alisema matukio ya ukatili wa kijinsia kwa Watoto yanatisha na takwimu siyo nzuri.

# Wanawake wachimbaji madini waomba kutengewa maeneo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI madini wanawake wameiomba serikali kuwatengea maeneo ambayo watakuwa wakifanya shughuli ya uchimbaji, pamoja na kuwawezesha mitaji na vifaa vya kuchimbia ili wajikwamue kiuchumi.

Walitoa ombi hilo kwenye kongamano la wanawake ambao wanajishughulisha na sekta ya uzinduaji (mafuta, gesi asilia na madini), ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, liliolandaliwa na Taasisi ya Haki-Rasilimali na kufanyika mkoani Shinyanga.

Katibu wa Chama cha Wanawake Wachimbaji wa Madini na Uongezaji Thamani Madini (WIMO), Mhandisi Lightness Salema, alisema katika kuwezesha mwanamke kunufaika na sekta ya uzinduaji, wanapaswa kutengewa maeneo yao kwa ajili ya uchimbaji madini pamoja na kuwezeshwa mitaji na vifaa vya uchimbaji.

"Mikwamo ambayo tunakutana nayo sisi wanawake kwenye uchimbaji wa madini ni ukosefu wa mitaji na vifaa vya kuchimbia madini, tunaiomba serikali kupitia kongamano hili la wanawake katika sekta ya uzinduaji ituangalie kwa mapana zaidi na kutupatia mikopo na hata kututengea maeneo yetu ya uchimbaji madini,"alisema Salema.

Kaimu Meneja Tathmini na Ufuatiliaji kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Oswald Karadisi, alisema katika baraza hilo kuna fursa mbalimbali za uwezeshaji.

Alisema kuna mifuko 73 ambayo inatoa ruzuku, mikopo ya moja kwa moja na dhamana na kuwataka wanawake wachimbaji wa madini wadogo wachangamkie fursa hiyo na kupata mitaji.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, aliwapongeza wanawake kwa kujishughulisha na uchimbaji wa madini, akisema sekta hiyo ilikuwa ikiaminika kuwa inawezwa na wanaume, lakini wao wamedhihirisha wanaweza kufanya shughuli hiyo.

Hivyo, alitoa wito Tume na Wizara ya Madini pamoja na taasisi za kifedha hapa nchini kuwaunga mkono wanawake ambao wanajishughulisha kwenye uchimbaji wa madini, ikiwamo kuwapatia mikopo ili wapate mitaji na kununua vifaa vya kisasa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Haki Rasilimali, Adam Anthony, alisema wameendesha kongamano katika sekta ya uzinduaji ili kujadili matatizo ambayo huwakabili na kuyatafutia ufumbuzi.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita (wa pili kulia), akikabidhi funguo ya pikipiki kwa Ofisa Ugani wa Kata ya Malunga, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Laibelia Sabini jana, zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuwatembelea wakulima na kuwapatia elimu ya kulima kitaalamu na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Maofisa ugani Sengerema, Ushetu wamepewa pikipiki

**Na Waandishi Wetu**

MAOFISA ugani kutoka Halmashauri ya Sengerema mkoani Mwanza na Ushetu mkoani Shinyanga wamepewa pikipiki 121, huku wakitakiwa kuzitumia pikipiki hizo kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa pikipiki hizo, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wilaya ya Sengerema imepokea pikipiki 83.

Alisema pikipiki zingine walipatiwa maofisa watendaji wa kata ambao waliahidi kuendelea kutoa huduma kwa wananchi ili kuhakikisha wanafikia lengo la serikali pamoja na kuinua kipato cha mtu mmoja.

Maofisa hao walisema walikuwa wanashindwa kuwafikia wananchi kwa wakati pindi walipohitajika kwenda kuwatatulia matatizo yao na kusababisha kukwamisha maendeleo kwa jamii husika.

Kadhalika, mkoani Shinyanga Halmashauri ya Ushetu pikipiki 44 zilitolewa, kati ya hizo 38 kwa ajili ya maofisa ugani na sita kwa watendaji wa Kata.

Aidha, kati ya pikipiki hizo 38 na halmashauri hiyo kwa kiwango kikubwa inategemea mapato yake ya ndani katika kilimo hususani cha tumbaku na pamba licha ya kuwa na mgodi mdogo wa madini ya dhahabu wa Mwabomba.

Kadhalika, halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inatarajia kukusanya na kutumia Sh. bilioni 32.6 kati ya hizo Sh. bilioni 3.4 ni mapato ya ndani na Sh. bilioni 29.1 ni ruzuku na fedha za wahisani ikilinganishwa na mwaka 2021/2022 walipanga kukusanya Sh. bilioni 31.1.

Akikabidhi pikipiki hizo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala, alisema vyombo hivyo vinatakiwa kutumika katika matumizi yaliyopangwa na siyo vinginevyo na atakayebainika kwenda kinyume na matumizi atawajibishwa kisheria.

Mbunge wa Ushetu, Emmanule Cherehani, alisema pikipiki hizo zitakatumike katika kudhibiti mapato yatokanayo na kilimo kwa sababu baadhi ya wakulima wamekuwa na tabia ya kutorosha mazao na kwenda kuuza wilaya za jirani zilizopo mkoani Tabora, Kigoma na Geita.


**Imeandaliwa na Elizabeth Seleman (Sengerema), Shabani Njia (Kahama)**

ama
ALHAMISI MACHI 9, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



## CCBRT Moshi yahesabu miaka 25 kuwafikia wenye ulemavu 18,000

Ukurasa 14



## Ujue ugonjwa uitwao 'maradhi adimu' unaotesa watoto kwa hali na gharama

Ukurasa 13

### MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA...

# Asivyo na masihara kwenye kumtua mama ndoo kichwani

• Msimamo tangu mawaziri wa kwanza...

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA wasifu unaobaki rekodi baada ya kuingia madarakani, ni pale akautajia umma safu ya watendaji wake wakuu wanaoapishwa ilisikika jina la Jumaa Aweso, kukabidhiwa Wizara ya Maji.

Ni utambulisho wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, uliomfikia mbunge huyo wa Pangani, kwa salamu zilizogusa utashi wa umma, akimpa tahadhari ya mapema "ukinizingua nitakuzungua..." kwa maana ya kamkabidhi chombo nyeti cha umma na hahitaji masihara.

Kimsingi, Dk Samia, muumini wa itikadi 'kumtua mama ndoo kichwani' ni mbia wa sekta ya maji, hali kadhalika mazingira, kwani hata alipokuwa Makamu wa Rais, mwaka 2016, akawa mgeni rasmi, kufungua Mkutano Mkuu wa 10 wa Baraza la Mawaziri wa Maji Afrika (AMCOW) jijini Dar es Salaam.

Ni mkutano uliohudhuriwa na Rais Mstaafu wa Kenya, Marehemu Mwai Kibaki, akiwa mjumbe maalumu wa UNESCO kuhusu masuala ya Maji na Usafi wa Mazingira, kuwa washiriki zaidi ya 1,500, wakiwamo mawaziri 26 wa maji.

Kimsingi, aina ya utani kutoka kwa Rais Dk. Samia, kiitifaki una sura ya kiafande, anapoelekeza jambo kimasihara, mdogo anafurahi, huku akipiga saluti ya kupokea ujumbe wenye sura ya amri.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, siku alipozindua chanzo cha maji Kigamboni, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

Ni utani kazini ambao sasa wengi wamekuwa wakimfuatilia Waziri Aweso, kama kuna mahali anajikwaa akaangukia hata 'akazinguliwa', maana kwenye sekta hiyo, panapo shida utashi wa kirafiki wa Dk. Samia unakaa kando; 'maji ni uhai' imebeba roho za Watanzania.

Upande wake Waziri Aweso amedhihirisha kukidhi mahitaji ya mkuu wa nchi, akiendelea kupatumikia akiidhinisha ridhaa ya Rais, hadi leo inatimu miaka miwili ya Rais madarakani.

Kama alivyozoea kutamka, James Mbatia, kiongozi muasisi wa chama - NCCR Mageuzi, kila hoja inapaswa kubeba kielezo, uhalisia, uchapa kazi wa Aweso, unasafiri hadi kwenye tukio la uzinduzi wa Skimu ya Maji ya Kakonko kata za; Kiziguzigu, mkoani Kigoma, Oktoba mwaka jana, inayotekelezwa kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Rais Dk. Samia anatamka kuwapongeza watumishi wa mradi wenzao, akiwasifu kwa usimamizi bora, kuyaona mabadiliko chanya Wizara ya Maji yanayotoa matumaini kuwa serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa na sekta hiyo.

"Zamani huko nilikuwa na ugomvi na watu wa maji. Kwa sasa, watu wa maji ni marafiki zangu kweli kweli, wizara imebadilika. Taasisi zilizoko chini ya wizara zimebadilika. Kazi inafanywa kweli kweli! Naomba muendelee hivyo hivyo," anasema Rais Samia.

Kimsingi ni skimu inayotekelezwa na RUWASA kwa kushirikiana na Ubelgiji, ikigharimu zaidi ya shilingi bilioni nne na inatarajiwa kunufaisha kata nne, ikiwa na jumla ya vijiji 14.

Katika kumkaribisha Rais Dk. Samia, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, anasema mradi unawagusa wakazi wapatao 65,010 na penye upanuzi wake utafikia jumla ya wakazi 132,425, mwaka 2042.

Kitaalamu akaeleza imeongeza upatikanaji maji kutoka asilimia 51 hadi zaidi ya asilimia 70, mgao wake ukipungua kutoka saa 12 hadi saa tano kwa siku.

Ni aina ya wasifu sasa Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, naye Oktoba mwaka jana, akaangukia hoja kama ya Rais wa sasa, akiwatamkia "RUWASA inafanya kazi nzuri ya kuwapatia wananchi waishio maneno ya vijijini majisafi na salama."

Hata Rais Mstaafu Kikwete, alizuru Wiki ya Uwekezaji na Biashara Mkoa wa Pwani, kwenye maonyesho ya Viwanja vya Stendi ya Zamani ya Kibaha Maili Moja, mkoani Pwani, pale alipopata taarifa kuhusu mwelekeo wa RUWASA, miradi ya maji na kuboresha kazi yao.

Mwishoni mwa mwaka jana, Rais Dk. Samia akakagua miradi ya maji, safari hiyo akiwa mkoani Pwani, baada ya kuwapo ukame wa vyanzo na shida ya maji, ambako akatoa maagizo ya kitaifa, akiwa katika vyanzo vya maji Ruvu, marufuku ya ukiukwaji utaratibu wa kunywesha mifugo na kutumia vyanzo vya maji katika maeneo hayo.

**AZINDUA MAJI KIGAMBONI**

Mnamo Novemba mwaka jana Rais Dk. Samia akazindua mradi wa Maji Kigamboni, mkoani Dar es Salaam kwa kuwasha mtambo wa kutoa maji ardhini, kwenye kisima kirefu mita 450, kwa ajili ya kuyapeleka kwenda kwenye tanki kubwa la maji eneo la Kigamboni, Dar es Salaam.

Hapo Kigamboni, akaahidi kuimarisha huduma ya maji katika

Inaendelea Uk. 14

AFYA

## VUGUVUGU SIKU YA WANAWAKE...

# Mwanamama Profesa Muhimbili, ashuhudia alivyofikwa na kansa na kupambana nayo

**Na Mwandishi Wetu**

MADAKTARI wanawake wawili katika kuadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani, wametoa ushuhuda wa namna ya kupambana na saratani ya matiti, ambayo imewapata. Wanaishi na wanaamini kuwa yeyote anaweza kupata maradhi hayo.

Jana kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, ilikuwa na simulizi ya Dk. Grace Mzengi, mtaalamu tiba anayeumwa.

Leo inamhusu Profesa Mshiriki, Julie Makani, bingwa tiba wa afya ya damu, kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), ana neno la tumaini kwa wanaoishi na saratani, akisema kufuatilia tiba ilivyo muhimu, kuikabili kansa.

Anaeleza chimbuko la mkasa huo, ilikuwa asubuhi Ijumaa ya Machi mwaka 2021, akiwa na umri miaka 51, pale alipoamka asubuhi na kuona tone la damu kwenye shuka chini ya matiti. Lakini, haikumuingia akilini, ungekuwa mwanzo wa kubadilisha maisha yake.

Anasimulia akashangaa jinsi ilivyotokea, kisha akakimbilia kwenye mkutano mtandaoni. Hakufikiria sana, akaendelea na mkutano. Profesa Julie anaendelea: "Nilihisi kulowana zaidi, kwani damu ilikuwa ikinitoka nyingi kwenye titi. Ilinishtua, nikampigia simu daktari wangu, aliyenishauri nikutane naye mara moja,"

Hapo anafafanua wanawake wengi hawapati matibabu ya haraka na wengine hupuuza dalili hadi hali inapokuwa mbaya.

Kwake ni bahati kugundua tatizo hilo mapema na kupata matibabu ya haraka, akiwa katika fani ya tiba.



Profesa Julie Makani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

### DAKTARI KAWA MGONJWA

"Ni hali iliyokuwa ngumu sana kwangu kuwa mgonjwa, kwa sababu sikuweza kuizima akili ya kidaktari au mwanasayansi anayefahamu kila kitu kuhusu kansa, halafu kama mgonjwa unakuwa katika hali ambayo unatamani usiwe nayo." anaeleza Profesa Julie.

"Nikiwa daktari bingwa na mwandamizi kuliko wale wanaonihudumia, tena wanaonijua kama mhadhiri wao, nilifadhaika sana, kwa sababu madaktari walionitibu walikuwa na wasiwasi sana au kuniogopa.

"Wapo walioniuliza 'ninafikiria nini.' Kama daktari, huwezi kubadili jukumu hilo, unasoma juu tatizo na kupata maoni kutoka kwa wenzako," anasimulia mtaalamu huyo.

Anafafanua kwamba katika kupata matibabu, alitambua upungufu, jambo ambalo mara nyingi inagusa mfululizo wa michakato ya uchunguzi tiba, mgonjwa anapaswa kupitia, iwapo anahisiwa kuwa na saratani ya matiti, kabla ya kutambua na kuthibitisha.

Profesa Julie anahoji iwapo aliwahi kuwa na uvimbe wa matiti awali, jibu lake likawa hapana.

### MWANZO WA TIBA

Anasema alipokutana na daktari wake, uchunguzi wa matiti ulichukuliwa na mtaalamu wa 'radiolojia' aliyegundua hali isiyo ya kawaida. Alipangiwa kufanyiwa uchunguzi wa 'ultra sound' ya matiti na 'mammography' siku iliyofuata; vyote vikaeleza zaidi hali isiyo shwari, kuna tatizo.

Daktari akapendekeza apatiwe uchunguzi wa sindano kupitishwa kwenye ziwa, ili kupata 'tishu' za ndani ya ziwa, inayojumuisha kutumia bomba refu kupata sampuli ya tishu kuichunguza.

"Ilichukua mwezi mmoja kupata matokeo ya ugonjwa. Hii ilinifanya kutafakari na kufikia wengine, kwa sababu kwangu ilichukua mwezi tena niko Muhimbili na nina nafasi ya kutibiwa. Vipi kuhusu ambaye hawezi kupata huduma kama yule anayetoka maeneo ya mbali zaidi mikoani? Hili lilinifanya nisisimke usiku na kuwaza sana."

Anasema, kupata matibabu kirahisi kama ilivyokuwa kwake ni bahati ya tatu, akiamini kinyume na hapo, pasikokuwa Muhimbili, akiamini huenda kungekuwapo ucheleweshaji zaidi.

"Uchunguzi ulichelewa na kwangu kama daktari niliona aibu kwa sababu nilijua nini kifanyike katika suala la uchunguzi. Lakini, naishukuru Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na Hospitali ya Agha Khan, kwa yote waliyofanya, utambuzi na matibabu wanayofanya," anaeleza bingwa huyo.

"Kwa kuona kilichotokea, ninagundua kuwa kuna mambo, au maelezo madogo muhimu ya kuongeza, ambayo yanaweza kuleta tofauti kubwa. Sehemu ya uchunguzi ni jambo muhimu. kwa sababu mara tu vipimo vinapofanywa, inakuongoza mara moja kwenye matibabu na kuzuia kuchelewa, ili kuondoa uwezekano wa mgonjwa kuwa na hali mbaya zaidi," anasema Profesa Julie.

Hapo ana mtazamo kwamba hilo linawaletea wagonjwa wengi hili linaleta kizuizi kikubwa; hatimaye wangeshangaa katika mfumo wa afya. Uchunguzi unaonyesha, ucheleweshaji wa matokeo ya vipimo, yanachukua wastani takriban mwaka mmoja, au siku 358. Cha kwanza muhimu, anataja ni kuitambua saratani.

Upungufu mwingine anautaja, wapo wanaoamua kutafuta tiba mbadala kwa waganga wa kienyeji, kukabiliana na vizuizi vilivyopo vya mfumo wa afya.

Saratani ya matiti inatajwa kuwa ya pili kwa wingi wa kansa kwa wanawake nchini na ya pili kuchangia vifo vya saratani miongoni mwa wanawake.

Inakadiriwa, kuanzia mwaka 2012 hadi 2030, idadi ya wagonjwa wapya wa saratani ya matiti Tanzania itaongezeka kwa asilimia 82 na idadi ya vifo vyake vitafikia asilimia 80.

Anaeleza namna alivyopewa mbinu nyingi za kukabiliana na ugonjwa huo, kutoka kwa marafiki, wafanyakazi wenzake na wanafamilia. Profesa Julie:

"Nafikiri jambo jingine lililotokea ni kupewa mawazo mengi mfano kutumia dawa vyakula na mimea fulani, kwenda kwenye maombi au kukutana na mchungaji, kuelekezwa sehemu ambayo ningeweza kujiunga na kuomba.

"Niliambiwa na madaktari wangu, pia wafanyakazi wenzangu. Hiyo ilinifanya nifikirie sana kuhusu wengine ambao hawakuweza kutambua habari hii na kuchagua la kufanya. Mara nyingi hiki ni kipindi kigumu sana." anaeleza.

### SAFARI NDEFU YA MATIBABU

Profesa Julie anaitaja kuwa ni safari ndefu kutoka uchunguzi hadi matibabu kwa mgonjwa wa saratani, ikiendana na hofu, kiwewe, msukosuko wa mihemko, uzoefu unaombatana na Mfululizo wa vipimo na tiba.

Profesa Julie, anafafanua:"Niliendelea kufikiria jinsi wagonjwa wengine wanavyofanya, kwa sababu mchakato mzima ulikuwa mgumu, ni rahisi sana mtu kukata tamaa, pia hufungua mwanya wa rushwa na uzembe."

Mtalamu huyo anaeleza kuwa tiba yake anaipata nchini Afrika Kusini, yalikopendekezwa na wafanyakazi wenzake, akieleza "nilitibiwa na mtaalamu bingwa wa upasuaji saratani ya matiti, huwafanyia upasuaji wagonjwa 20 kwa siku. "

Anayemtibu, mtaalamu mwandamizi wa radiolojia ya saratani ya matiti, akitamka huwa anasoma picha za wagonjwa karibu 100 kwa siku, akamfafanulia:"Niliona tofauti ya uzoefu na utaalamu waliokuwa nao wote wawili, jambo ambalo lilikuwa kinyume kabisa na hapa Tanzania."

Hapo anarejea ushuhuda wa mfumo wa afya katika nchi nyingine, Profesa Julie, ana mtazamo wa kuwekwa pamoja wataalamu wa taaluma nyingi na umuhimu wa kuwapo utaratibu wa dharura, kuwahudumia kikamilifu wagonjwa wa saratani.

Anaeleza alivyotibiwa: "Nilifanyiwa upasuaji wa kuhifadhi matiti. Ilibidi watoe sehemu ya titi langu lenye ugonjwa na daktari wa upasuaji alilazimika kuchukua sehemu kubwa ya lile zima, ili kuliunda upya kuyafanya yawe sawa, yasiyo na tofauti"

Anakumbuka, akapata matatizo kiafya yanayoitwa 'neutropenia' au uhaba wa chembe nyeupe zinazosaidia kinga. Pia, akaugua kutokana na kuchoma mionzi, ukiwa ni utaratibu wa kuzingatia, napo akachunguzwa mara moja, kwani kulikuwa na vifaa vya uchunguzi wa upasuaji, na matibabu yote yalipatikana.

Anakiri kushuhudia mfumo uliojengeka, akiamini toba hiyopkuwa ndiyo imemuwezesha kuwa hai hadi sasa, licha ya saratani yake kuwa katika hatua za awali.

Daktari huyo, anasema anaendeleza matumaini ya uhai wake, akidumisha sala kumtegemea Mungu kiimani.

*• **Makala hii kwa mujibu wa MEDICOPRESS .***

AFYA

# Ujue ugonjwa uitwao 'maradhi adimu' unaotesa watoto kwa hali na gharama

**Na Elizabeth Zaya**

SIKU za Magonjwa Adimu Duniani huadhimishwa kila Februari 28 ya mwaka, lengo ni kujenga uelewa miongoni mwa jamii, kuhusu magonjwa yanayotokea kwa kundi dogo la watu, hususani watoto, yakipewa jina 'magonjwa adimu.'

Daktari Bingwa wa Watoto, Mariam Noorani, anasema magonjwa adimu ni yale yanayotokea kwa nadra na kwa wagonjwa wachache sana duniani.

Zipo changamoto nyingi zinatajwa za kidini, kihisia, kiuchumi na kijamii katika kuyatambua magonjwa hayo kwa wanaoishi nayo, huku jamii ikikosa elimu ya kutosha kuhusu undani wake.

Kurejea wataalamu wa afya, asilimia 72 ya magonjwa hayo yanatokana na vinasaba na zaidi ya asilimia 70 ya wanaokumbwa nayo, ni watoto wadogo, ikitajwa kuwaathiri kwenye ubongo, damu na ini.

Kutokana na jamii kukosa uelewa wa kutosha wa ugonjwa huo, haiupi kipaumbele kutokana na ufahamu mdogo walio nao, ukosefu wa tafiti makini kutokana na ukata wa rasilimali fedha na vifaa tiba.

Nchini Tanzania, serikali sasa inaweka mikakati yake ya kuhakikisha inasimamia kikamilifu na kuweka mazingira mazuri ya kisera kuhakikisha watoto wenye magonjwa adimu, wanapatiwa haki sawa na kutoachwa nyuma katika kuhudumiwa.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipohutubia taifa baada ya kuapishwa, akasisitiza kuhusu serikali yake kuweka mipango maalum kuhudumia makundi yenye magonjwa adimu.

Miongoni mwa maeneo hayo, serikali imeboresha katika sekta ya elimu, kuhakikisha watoto hao wanafuatwa majumbani na kupatiwa elimu kama ilivyo kwa wengine.

Sharifa Mbarak, mama mwenye mtoto anayeishi na magonjwa adimu, anasema licha ya serikali kuendelea kuweka mipango mizuri kwa watoto hao bado wanapata shida kwenye upatikanaji wa huduma eneo la sekta ya afya.

Anasimulia kwamba watoto wanaosumbuliwa na ugonjwa huo hutumia gharama kubwa ya matibabu kwa sababu, tiba yake inapatikana kwenye hospitali kubwa, kutokana na uhitaji vifaa na vipimo vinavyopatikana huko pekee.

Sharifa anasema, ni ugonjwa unaotakiwa kutumia mashine za kupumua na kuongezwa oksijeni muda wote kwa baadhi yao, hata upatikanaji wake unakuwa na urasimu mkubwa, mtu wa kawaida anashindwa kulipia gharama zake.

Akitoa mfano wa mwanawe, Ally Kimara, mama huyo anasema mwanae hutumia mashine au kuongezewa oksijeni muda wote na anapotumia mashine gharama yake si chini ya Sh.50,000 kila siku.

"Nikisema leo tuongeze oksijeni, ambao mtungi lita 15 ukitumia miwili kwa saa 24 ni Sh. 80,000, kila mtungi mmoja ni Sh. 40,000, utaona hapo ni namna gani gharama inakuwa kubwa kwa wagonjwa hawa," anasema.

"Tunaomba serikali iangalie haya tunayopitia katika sekta ya afya, siyo rahisi kumudu kwa kipato chetu tunachokipata, wazazi wenye watoto kama hawa, wanapunguza au wanaacha kabisa kufanya kazi, ili waweze kuwahudumia watoto na hii inafanya kipato chao cha kawaida kinazidi kushuka na kushindwa kuwahudumia," anaeleza.

Anasisitiza kwamba, hakuna mtu anayelipia pumzi, bali wote wanapumua, hivyo anatoa wito kwa serikali, kuwaangalia watoto hao ambao ni wachache wanaotumia oksijeni ya ziada, ikizingatiwa ndio tegemeo lao.

"Tungeomba serikali iangalie uwezekano wa kutoa oksijeni bure kwa watoto hawa au ikishindikana kabisa, gharama zipunguzwe ili kila mzazi na anayelea mtoto wa namna hii amudu.

"Tunaishukuru serikali kupitia Rais Samia kwa jitihada zake kwa watoto hawa na tumeona tangu alipokuwa Makamu wa Rais hadi nafasi aliyo nayo sasa, alivyokuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha anawawekea mazingira mazuri watoto hawa, ni yeye aliyesema wapatiwe elimu kwa kufuatwa majumbani.

"Hivi mtoto wangu anakuja kufundishwa na mwalimu wake hapa nyumbani, ambaye ameletwa na serikali na alifanya mtihani wake wa darasa la nne na matokeo yake ni mazuri amepata alama 'A'. Kwa hiyo, naomba na watoto wengine wote nao wapate neema hii na haki yao ya msingi," anaeleza Sharifa.

Anasema, tangu mwaka 2021 walipofanya maadhimisho ya kwanza nchini Tanzania ya Siku ya Magonjwa Adimu na kuanza kuongeza uelewa kwa jamii, wameanza kuona matokeo chanya.

"Japokuwa elimu bado haijafika kwa upana wake kwa umma, lengo letu ni kutaka ifike hadi vijijini. Imani za kishirikina watu wasiziweke, unapoona mtoto wako ana dalili ambazo hazipo sawa mpeleke hospitali," anasema Sharifa.

Anaongeza: "Pia tunashukuru Wizara ya elimu kupitia 'foundation' (Mfuko) yetu ya Ally Kimara Rise Disease, kufanya mikakati jumuishi, hawa watoto katika kuwapatia elimu na sasa hivi wanaandaa muongozo ambao utawajumuisha katika mambo mbalimbali."

Mama huyo anafafanua, katika bajeti ya mwaka 2021/22 ya Wizara ya Afya, ilitaja kundi la watoto waishio na magonjwa adimu, ikiwaingiza katika bajeti ya kuwahudumia , hata kuwapa matumaini.

**DAKTARI BINGWA**

Tabibu Bingwa wa Watoto na Mkuu wa Idara ya Watoto Hospitali ya Aghakhan nchini, Dk. Mariam Noorani, anayafafanua magonjwa adimu ni yanatokea kwa nadra na kwa wagonjwa wachache duniani.

"Ndio maana ni vigumu kuyatambua na kuyafahamu katika jamii na huku ndiko husababisha baadhi ya wazazi au walezi kuwa na imani potofu.

"Kutokana na magonjwa haya kuwa magumu kutambulika, hata baadhi ya madaktari huyachanganya na hata kupata changamoto namna ya kuyatibu au kuyaelezea kwa jamii kwenye lugha inayoeleweka.

"Kwa hiyo, tunaendelea kupaza sauti kwa wataalamu wa Afya, serikali na jamii ili wafahamu kwamba haya ni magonjwa yapo, licha ya changamoto nyingi zilizopo.

Anaeleza changamoto nyingine inayowakabili wenye ugonjwa huo, ni upatikanaji wa huduma za vipimo na dawa, anayoisema haipatikani kwa urahisi nchini.


"Hivi ndivyo vinachangia kwa kiwango kikubwa kuwahudumia watoto wa namna hii, kuwe kugumu na kwa gharama kubwa zaidi," anasema Dk. Miriam.

Anasisitiza rai kwa serikali iendelee kusaidia na kuhamasisha kupunguzwa gharama kwa wagonjwa hao, kwani ni kubwa sana katika matibabu.

Mtalamu huyo anataja kuwa, ni hivi karibuni watoto wenye magonjwa adimu, wanapatiwa matibabu katika hospitali tofauti na ilivyokuwa zamani, jambo ambalo ni la faraja.



Mgonjwa Ally Kimara, akifundishwa nyumbani, huduma maalum anayopewa ya kufuatwa na mwalimu.



Ali Kimara, akijifunza nyumbani. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA.**

AFYA

# CCBRT Moshi yahesabu miaka 25 kuwafikia wenye ulemavu 18,000

**Na Margaret Malisa**

SIKU ya Februari 25 mwaka huu, Hospitali ya CCBRT ya Dar es Salaam, ilisherehekea miaka 25 ya kutoa huduma za utengemao wa Kanda ya Kaskazini na maeneo mengine nchini kupitia kituo chake cha CCBRT Moshi maarufu 'Nyumba ya Matumaini.'

Makao yake makuu Msasani Dar es Salaam, yalianzishwa kama programu ya kijamii mwaka 1994, kwa lengo la kutoa tiba kwa wagonjwa wa macho, hususan mtoto wa jicho na magonjwa mengine ya macho yanayosababisha upofu unaozuilika.



Wagonjwa wanaohudumiwa katika kituo cha CCBRT, mjini Moshi. **PICHA: MARGARET MALISA.**

Baada ya mwaka 1996, likaanzishwa tawi la CCBRT Moshi maarufu kama 'Nyumba ya Matumaini' kutoa huduma za utengamao kwa watu wenye ulemavu na familia za Kanda ya Kaskazini na mikoa mingine.

Ni kituo kilichowezesha maelfu ya watu wenye ulemavu na familia zao, kupata huduma za utengamao, na kuboresha maisha yao.

Wanaohudumiwa kituoni hapo, ni pamoja na watoto wenye mtindio wa ubongo, vichwa vikubwa na mgongo wazi, miguu kifundo au nyayo zilizopinda, sambamba na wenye ulemavu wa viungo wanaohitaji huduma ya utengamao, viti mwendo na vifaa saidizi vinavyowawezesha kuendesha maisha yao kila siku.

### MKUU CCBRT

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT Brenda Msangi, anasema taasisi yake kwa kushirikiana na wadau, imeadhimisha siku hiyo ikitathmini mafanikio waliyofikia katika kuwahudumia wenye changamoto za ulemavu na wakati huohuo kutathmini changamoto walizokabiliana nazo kwa kipindi chote.

Anasema, kwa kushirikiana na serikali, CCBRT kupitia kituo caho imewezesha huduma za utengamao kwa maelfu ya watoto wenye ulemavu na familia zao.

Pia anataja mikoa mingine huduma inakolewa sasa, ni katika mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Tanga, Dodoma, Iringa, Shinyanga, Kigoma Mwanza na Morogoro.

Kituoni CCBRT Moshi, watoto wenye ulemavu hupatiwa matibabu ya kina wakati wa wiki maalumu ya mazoezi tiba (Week of Intensive Treatment).

Brenda anadems, programu hiyo inajumuisha wiki nzima ya mazoezi tiba kwa watoto na jopo la wataalamu (Daktari wa watoto, Fiziothearapia, Watalaamu wa tiba kwa vitendo (Occupational Therapists) na mtaalamu wa lishe) wanapata muda wa kutosha kuwahudumia watoto hawa.

Pia anataja kuwapo kliniki ya vifaa tiba, mafunzo juu ya lishe na baada ya wiki maalumu ya mazoezi watoa huduma majumbani na wataalamu wanamfuatilia mteja kwenye jamii, kuwapatia mafunzo mbalimbali ikiwemo jinsi ya kujikwamua kiuchumi, matumizi sahihi ya vifaa na, uangalizi wa vifaa vyao saidizi.

Huduma nyingine zinazotolewa na kituo hicho ni huduma kwa watoto wachanga waliozaliwa na miguu kifundo, kliniki ya wateja wa kutwa, kliniki ya viti mwendo/vifaa tiba ambayo wahitaji hutengenezewa vifaa hivi kulingana na uhitaji wao.

Kwa kushirikiana na wadau kama vile maofisa elimu maalum wa Halmashauri ya Moshi, watoto wenye ulemavu wameandikishwa shule za kawaida na kujumuika na wasiokuwa na ulemavu, baada ya kupata huduma za utengamao na vifaa tiba saidizi.

Anasema, CCBRT kupitia kituo hicho, kwa kushirikiana na serikali; Idara ya Maendeleo ya Jamii na Mashirika /Taasisi zinazotoa mikopo na elimu ya ujasiriamali wameziwezesha familia na walezi wenye watoto wenye ulemavu, kuanzisha biashara ndogo na kujikwamua kiuchumi.

### MAFANIKIO YALIVYO

Brenda anataja baadhi ya mafaniko ya kituo chake kwa miaka 25 ni kuwafikia wenye ulemavu zaidi ya 18,000; vifaa saidizi 10,000 vimetolewa kwa kada hoyo ya jamii; viti mwendo 3,500 vimetolewa.

Lingine, ni kuboresha uchumi wa familia kutoa mafunzo kwa wadau na wafanyakazi wa afya wa serikali zaidi ya 12,000 na kuongeza ubora wa huduma na upatikanaji wataalamu wa huduma za utengamao.

CCBRT kwa kushirikiana na wizara na wadau imewezesha serikali ya Tanzania kuwa na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Huduma za Utengamao (National Rehabilitation Strategy) uliozinduliwa Mwaka 2021, kusaidia mifumo ya utoaji huduma za afya na masuala ya watu wenye ulemavu kuwa jumuishi.

Hadi sasa kuna mnufaika wa muda wa mrefu wa huduma za utengamao kutoka CCBRT Moshi, Emmaneul Kipingu (28), mlemavu wa viungo mwenye mtindio wa ubongo.

### CHANGAMOTO ZILIZOKO

Mkurugenzi Brenda, anaeleza kituo hicho kinakabiliwa na changamoto nyingi, akiziorodhesha:

- Utegemezi wa wafadhili wa nje.
- Gharama kubwa na upatikanaji wa shida wa vifaa tiba kwa wahitaji.
- Uchumi duni kwa familia za watoto wenye ulemavu, husababisha watoto kushindwa kupata huduma stahiki na wakati.
- Miundombinu ya ofisi, shule, hospitali na vyombo vya usafiri siyo rafiki, changamoto hasa kwa watumiaji ifaa saidizi kama viti mwendo.
- Wataalamu ni wachache kuhudumia utengamao
- Hakuna barabara rasmi ya kuingia kituoni CCBRT Moshi na hata watoto

# Asivyo na masihara kwenye kumtua mama ndoo kichwani

**INATOKA UK. 11**

wilaya za Temeke, Ilala na Kinondoni, kupunguza makali wa mgao wa maji, majibu yaliyoshuhudiwa ndani ya muda mfupi.

Ni siku hiyo, Rais Dk. Samia, akiagiza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kuhakikisha inasambaza maji kwa wananchi katika wilaya ya Kigamboni kwa asilimia 100.

Hapo anaitaka Wizara ya Maji kutoa elimu kwa wananchi, kuacha kuchoma misitu ovyo, kuchepusha maji na kuingiza mifugo, hasa kwa wananchi wanaoishi kando ya vyanzo vya maji, akikumbusha inachangia upungufu wa maji.

Rais, pia akaahidi serikali ingetekeleza ujenzi wa Bwawa la Maji la Kidunda mkoani Morogoro, litakalotumika kukusanya maji wakati wa mvua, akisema ni wakati wa kukabidhi mitambo ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa na eneo kwa mkandarasi wa Mradi wa Bwawa la Maji la Kidunda.

Anasema, bwawa hilo lenye thamani ya shilingi bilioni 329 litakalojengwa kwa kutumia fedha za ndani, litawezesha uhakika wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima jijini Dar es Salaam na maeneo ya mkoa wa Pwani. yanategemea maji ya Mto Ruvu.

Ujenzi wa bwawa utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka jana na kukamilika 2025, ikiaminika utachochea maendeleo ya viwanda mkoani Pwani na Dar es Salaam.

### MAMA ASAIDIWA

Suala la maji na huduma yake inajishuhudia, hata pale wakati fulani mwaka huu, Mtendaji Mkuu wa Serikali, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwa wilayani Mpanda, mkoa wa Katavi, akafika hapo na kucharuka dhidi ya mtendaji wa chombo cha maji ya umma, akihisi hujuma hata akalifikisha kwa vyombo vya dola, kwa utekelezaji kisheria.

Majaliwa anaenda mbali akitaja na uelewa wake katika hilo, akifafanua namna alivyomfuatilia mtendaji huyo kutoka kituo cha kazi mkoa mwingine alikokuwa anatumika na alishapambana naye.

Hapo inafungua picha, ya uhalisia pale mtendaji mkuu wa serikali anafuatilia sera ya 'mguu kwa mguu' kuhusu haki ya upataji maji safi na salama.

Ni katika hatua kama hiyo, Waziri Mkuu akiwa Kilwa, akamuagiza Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kilwa, kufanya utafiti utakaowezesha upatikanaji maji safi na salama, katika maeneo yote yenye changamoto ya maji katika wilaya hiyo.

Anatamka, Rais Dk. Samia amedhamiria kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana katika kila kijiji, ikiwa ni utekelezaji wa kampeni yake ya kumtua mama ndoo kichwani. Ilikuwa, Oktoba mwaka 2021.

"Utafiti lazima ufanyike ili tujue wapi tunapata maji, Rais Samia anatoa pesa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi, piteni mpime maeneo yote mtafute vyanzo na mtuambie maji yako kiasi gani, mitambo na wataalam tunao," anatamka Majaliwa

### SERA YA MAJI

"Maji ni muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Aidha maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa.

"Katika hali yake ya asili, maji ni sehemu ya mazingira ambapo wingi na ubora wake ndio unaosaidia katika kuamua jinsi maji yatakavyotumika. Upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na usafi wa mazingira ni muhimu katika kulinda afya za wananchi.

"Utumiaji wa maji ambayo sio salama na uhaba wa maji huchangia katika kusababisha milipuko na kuenea kwa magonjwa kama kuhara na kipindupindu. Japokuwa maji ni muhimu kwa uhai wa viumbe, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hakuna uwiano wa mgawanyo wa maji ulio sawa kati ya sehemu moja na nyingine na katika majira mbalimbali ya mwaka. Aidha, wingi wa maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi una kikomo, na maji hayo pia yanaweza kuathirika kirahisi".





## Wazazi wadaiwa kuwatelekeza watoto wenye ulemavu shuleni

**Na Ibrahim Joseph,** BAHI

OFISA Elimu Maalumu wa Wilaya ya Bahi, Sarah Chizingwa, amesema asilimia kubwa ya wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma katika Shule ya Msingi Viziwi ya Kigwe wilayani Bahi mkoani Dodoma wametelekezwa na wazazi wao.

Alyasema hayo juzi wakati akizungumza na kinamama wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA) walipotembelea shule hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Chizingwa, alisema asilimia kubwa ya wanafunzi wanaosoma shule hiyo wametelekezwa na wazazi wao baada ya kupelekwa hapo.

"Kinamama wenzangu wanafunzi hawa waliopo hapa asilimia kubwa wametelekezwa na wazazi wao na hapa siyo shule tu bali imekuwa ni sehemu ya nyumbani kwao pamoja na wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne,"alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na hilo shule hiyo pamoja na uongozi wa serikali wamekuwa wakiwasaidia mahitaji yao wanafunzi hao ili kutimiza ndoto zao za kupata elima.

Alisema baadhi ya wazazi hao wamekuwa wakiwapeleka watoto hao shuleni hapo kwa lengo la kupata masomo lakini baadaye huwatelekeza kutokana na ulemavu wao.

Kadhalika alisema wanafunzi hao wamekuwa wakifanya vizuri kwenye masomo yao na kuchaguliwa kujiunga na shule mbalimbali za sekondari nchini, lakini baada ya kuhitimu kidato cha nne wengi wamekuwa wakirudi shuleni hapo kwa sababu hawana sehemu ya kwenda.

Katibu wa kinamama wa DUWASA, Esta Mlewa alisema wametoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mlewa alisema wamekuwa na utaratibu wa kutoa misaada hiyo wakati wa maadhimisho hayo kila mwaka kwa maeneo mbalimbali nchini.

Alitaja vitu walivyokabidhi shuleni hapo kuwa ni sabuni, magodoro, mafuta ya kujipaka na kupikia, dawa za miswaki pamoja na taulo za kike vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 1.5.

Awali akitoa taarifa ya shule hiyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kigwe Viziwi, Thadei Mwagila alisema shule hiyo ina wanafunzi 112 kati ya hao wavulana ni 67 na wasichana 45.

Alibainisha matatizo yanayowakabili shule hiyo kuwa ni upungufu wa vifaa vya kufundishia masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mengine ni upungufu wa magodoro ya kulalia wanafunzi hao na uchakavu wa mabweni ya kulala.

Aliongeza kero nyingine ni aina ya mitihani wanayopimwa wakati wa kumaliza elimu ya msingi na sekondari kutokuwa rafiki kwa wenye ulemavu wa viziwi kwa sababu ya ujifunzaji wao kuwa na majibu ya mkato.

## TASAC, NBS wafanya sensa vyombo vya usafiri majini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwamo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais TAMISEMI imefanya sensa ya kwanza ya vyombo vidogo vya usafiri majini.

Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Kaimu Mkeyenge, alibainisha hayo jana jijini hapo wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na wakala huo katika kipindi cha miaka miwili.

Mkeyenge alisema katika sensa hiyo taarifa kuhusu vyombo, umiliki na mahali vilipo nchini zilikusanywa na kuingizwa katika kanzidata kwa malengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuboresha usimamizi wa usalama wa vyombo vya usafiri majini, utungaji wa sera na mipango itakayoongeza mchango wa uchumi wa rasilimali za maji katika pato la taifa.

"Sensa ya namna hii ni ya kwanza kufanyika nchini na itawafaidisha wadau mbalimbali walipo katika sekta hii ya usafirishaji wa njia ya maji,"alisema.

Aidha, alisema ili kukuza uwekezaji katika shughuli za usafiri majini na uvuvi, serikali kupitia TASAC inaendelea kukamilisha mradi wa kimataifa wa mawasiliano na uchukuzi katika Ziwa Victoria.

"Lengo la mradi huo pamoja na mambo mengine ni kujenga vituo vinne vya uokozi ambavyo vitakuwa kimoja kimoja katika maeneo ya Kanyala - Sengerema, Musoma - Mara, Nansio - Ukerewe na Ilemela - Mwanza ambavyo vitasaidia katika kushughulikia changamoto za usafiri kwa njia ya maji na katika uokozi majini, kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia maji na kuongeza fursa za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kandokando ya Ziwa Victoria," alisema Mketenge.

Kadhalika alisema mradi huo unaotekelezwa na nchi za Tanzania na Uganda na utagharimu Sh. bilioni 59.23, kwamba upande wa Tanzania gharama za mradi ni Sh. bilioni 19.97 zinazojumuisha gharama za kazi za ndani na sehemu ya mchango wa Tanzania katika kugharamia kazi za kikanda zinazofanywa kwa kushirikiana na Uganda.

Alisema TASAC inatekeleza miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) katika kuhakikisha manunuzi, matumizi bora, sahihi na salama ya vifaa na mifumo yote ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) serikalini.




Wanawake kutoka wizara, taasisi na idara mbalimbali wakishiriki maandamano ya Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika kimkoa katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Katibu CCM: Wanawake wanajukumu la kusimamia maadili katika jamii

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kongwa, Joyce Mkaugala, amesema wanawake wanajukumu la kusimamia maadili katika jamii kwa kuhusika kikamilifu kwenye malezi ya watoto pamoja na kuhakikisha wanakwenda shule.

Pia amewataka wanawake hao kunusuru maadili ya jamii ambayo kwa kiasi kikubwa yamemomonyoka.

Mkaugala alisema hayo jana kwenye maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, iliyoandaliwa na Divisheni ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na umoja wa walimu wanawake Wilaya ya Kongwa, yaliyofanyika Kata ya Mkoka.

Alisema wanawake wanajukumu kubwa katika kuhakikisha watoto wanapatiwa malezi bora ili kunusuru maadili ambayo yamemomonyoka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, aliwataja wanawake kusimamia mchakato wa maendeleo.

Pia alikabidhi vifaa mbalimbali vya usafi wa mwili na vyombo vya chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Mkoka vya Sh. 800,000 vilivyotokana na michango ya umoja wa walimu wanawake Kongwa na wadau mbalimbali.

Ofisa Elimu Maalum Wilaya ya Kongwa, Sophia Mohamed akizungumza kwa niaba ya wanawake kutoka Divisheni ya Maendeleo ya Jamii na Umoja wa Walimu alisisitiza jamii kupaza sauti kupinga ukatili wa kijinsia na unyanyasaji kwa watoto wakiwamo wenye mahitaji maalum.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Paskalina Duwe, aliwataka wanawake kuwa na mshikamano wa umoja wa walimu ikiwa na pamoja na kuendelea kusaidia makundi mengine ngazi ya jamii kama wanavyofanya kwa wanafunzi.

Duwe alitumia fursa hiyo kutoa wito wa kushiriki kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kimkoa ilifanyika wilayani Kondoa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkoka, Eliah Chibago, aliwahimiza wanawake kukemea vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vinavyotajwa kukithiri baina ya wanawake na wanaume.





# Ukosefu wa fedha NGO chanzo cha migongano ya majukumu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

UKOSEFU wa fedha kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) imesababisha migongano katika majukumu ya kazi kutokana na mashirika mengi kutekeleza shughuli ambazo hawajapewa kibali cha kuzifanya.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango, Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Kilundo, alitoa kauli hiyo alipofungua mafunzo ya siku moja ya kuwajengea uwezo mashirika 60 yasiyo ya kiserikali mkoani Mbeya.

Kilundo alisema mashirika mengi yamekuwa yakiomba usajili kwa ajili ya kutekeleza shughuli f ulani za kijamii lakini wanapohitaji fedha hukiuka sheria na miongozo waliyopewa wakati wa usajili kwa kutekeleza shughuli zilizo nje ya usajili wao kwa lengo la kupata fedha.

"Mashirika yanapata fedha kwa uandishi wa maandiko, kwa hiyo mfano alisajili kuhudumia watoto yatima lakini anaona tangazo limetolewa wanawezesha masuala ya kidemokrasia hivyo anaandika andiko akipata fedha anajikuta anatekeleza kitu ambacho hajapewa kibali na mwisho inaleta mgongano na wengine wanaofanya kitu kama hicho,"alisema Kilundo.

Aliongeza kuwa mashirika mengi hayawasilishi taarifa zao kila baada ya miezi mitatu kutokana na wengi kupuuza sheria na miongozo iliyowekwa na wengine kwa kisingizio cha kuwa hawakutekeleza kazi zao.

Ofisa Mwandamizi kutoka Shirika la FCS ambao ni waandaaji wa mafunzo hayo, Nicholaus Mhozya, alisema wanawajengea uwezo mashirika hayo kutokana na baadhi ya upungufu ambao wameubaini katika uendeshaji wa mashirika ikiwamo uelewa mdogo wa sheria na miongozo ya ulipaji kodi inayosimamia mashirika hayo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema vikwazo wanavyokutana navyo ni ukosefu wa fedha za ufadhili kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao hali inayoleta changamoto katika ulipaji wa kodi.

Mashirika 60 yasiyo ya kiserikali mkoani Mbeya yamejengewa uwezo kuhusu sheria za mashirika, ulipaji kodi pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya mashirika hayo na serikali, mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika la FCS, Baraza la Asasi zisizo za serikali Taifa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.




Mkurugenzi wa masuala ya Sheria na Udhamini wa Wanawake wa Kampuni ya Serengeti Breweries Ltd, Lucia Minde (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Wafanyabiashara Wadogo wa Airtel Tanzania, Alice Mashiku (wa pili kushoto), wakikabidhi kifaa cha intaneti isiyo na kikomo kwa wanafunzi wanawake wa mambo ya kibunifu ya teknolojia wa kampuni bunifu ya Lauchpad Tanzania, wakati wa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Viongozi Songwe watakiwa kusimamia barabara kimkakati

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, amewataka viongozi wa Mkoa wa Songwe kubeba ajenda ya barabara za kimkakati ambazo zinachangia ukuaji wa uchumi wa mkoa.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye kikao cha bodi ya barabara kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe.

Alisema kuna barabara nyingi ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Songwe, hivyo viongozi lazima wahakikishe ajenda ya barabara inakuwa kipaumbele.

"Kucheleweshwa kwa barabara hizo kunapoteza mapato kwa mfano Barabara ya Mlowo - Kamsamba ni moja ya barabara muhimu katika kukuza uchumi kwa sababu ni kiungo cha mikoa miwili Songwe na Rukwa ambayo ukikamilika ujenzi wake ambao ni kiwango cha lami utaongeza mapato yetu," alisema Mhandisi Kasekenya.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanafungua barabara zote ambazo zinaunganisha mitaa na vijiji ili kurahisisha shughuli za uzalishaji mali.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe, Neema Mwandabila, alisema haoni sababu ya kutochukuliwa hatua kwa makandarasi wanaoshindwa kutekeleza kazi na kusababisha wananchi kutopata huduma kwa wakati.

# Bil. 1.4/- zatengwa kuwalipa fidia wakazi wa Ndelezi

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Jenerali mstaafu, Venance Mabeyo, amesema serikali inatarajia kuwalipa fidia wananchi wa Kijiji cha Ndolezi mkoani Songwe waliothaminisha maeneo yao.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizindua makumbusho yaliyoko katika Kitongoji cha Isela Kijiji cha Ndolezi, Kata ya Mlangali wilayani Mbozi.

Alisema serikali imekusudia kulipa fidia kwa kaya 176, Sh. bilioni 1.4 ili wakajenge makazi mapya na kuacha eneo la makumbusho kuendelezwa.

"Serikali imekusudia kulipa Sh. bilioni 1.4 kwa wananchi waliopisha upanuzi wa kituo hiki, hivyo naomba mwendelee kuunga mkono jitihada hizi hadi sasa tumeshatenga fedha za kuanza kulipa fidia hizo," alisisitiza Jenerali mstaafu Mabeyo.

Alifafanua kuwa moja ya shabaha ya serikali ya kuzindua makumbusho hayo ni kuhakikisha fursa za kiuchumi zitapatikana kila pembe ya nchi ili kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kupitia sekta ya utalii.

Vile vile alitumia fursa hiyo kuwashukuru viongozi wa kimila kwa kutoa ushirikiano kuonyesha mila na desturi ya jamii inayokaa katika maeneo hayo na kusema kuwa makumbusho hayo ni ya kwanza ya aina yake kwa Nyanda za Juu Kusini.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk .Francis Michael, aliwataka NCAA kuendelea kufanya maboresho zaidi katika kituo hicho ili kuwavutia watalii wengi kutembelea eneo hilo.

Akitoa taarifa ya mkoa kuhusu utalii, alisema kuwa wanaendelea kuhifadhi na kuvitunza vivutio vya utalii ili kutopoteza uhalisia wake ambapo vivutio vilivyoko mkoani humo ni pamoja na Kimondo, chemchem ya maji moto, masalia ya maandaki ya vita kuu ya pili ya dunia pamoja na mapango ya popo.

Alitaja mengine ni maporomoko ya maji ya Mto Momba, Sange na Bwenda, jiwe lenye alama ya unyayo wa binadamu wa kale, michoro ya kale kwenye miamba, madaraja ya kuning'inia matanuru ya kale ya kufua vyuma majengo ya Kanisa Katoliki lililopo Wilayani Momba Mkulwe, Nagalula wilayani Songwe yenye miaka zaidi ya 120.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, George Msyani, alimuomba Mwenyekiti wa NCAA Jenerali Mstaafu Mabeyo kusimamia na kuweka msukumo wa haraka kulipwa fidia hiyo kwani kutolipwa kwa wakati kunaleta sura ya kudhulumiwa na hivyo kuichukia serikali.

Licha ya tamko la kulipwa fidia baadhi ya wananchi waliomba serikali iwatengee maeneo maalumu ya kujenga makazi yao mapya, huku wakidai kulipwa fidia bila kuwapa maeneo ya kujenga itakuwa siyo kuwatendea haki.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Joshua Mwankunda, alisema kuwapo kwa makumbusho hayo kutaleta chachu ya maendeleo.





# SMZ kutumia tril.1.06/- miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inakusudia kutumia asilimia 53.8 ya Sh. trilioni mbili (Sh. tril.1.06) katika miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari wa CCM, Khamis Mbeto Khamis, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya CCM Kisiwandui Zanzibar, kuhusu tuhuma mbalimbali zilizotolewa na Chama cha ACT-Wazalendo.

Alisema miradi inayotarajiwa kujengwa ni pamoja na hospitali za mikoa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa hospitali 12 ambazo zimejengwa kwa kila wilaya.

Alisema Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameamua kutoa kipaumbele maeneo ya huduma za jamii katika sekta ya afya, miundombinu, elimu na huduma za majisafi na salama.

Mbeto alisema serikali inaendelea na mpango wa kujenga bandari ya kisasa katika eneo la Mangapwani baada ya Bandari ya Malindi kukabiliwa na ufinyu na kushindwa mizigo kutoka kwa wakati.

Alisema serikali imenunua mashine za kupakia mizigo na kushusha za Sh. bilioni 18.4 ili kazi za uchunguzi na usafirishaji mizigo ziweze kufanyika kwa wakati katika bandari hiyo.

Alisema Bandari ya Malindi Unguja ilijengwa miaka ya 1990 wakati idadi ya watu Zanzibar ikikadiriwa kuwa 800,000 lakini kwa sasa sekta ya biashara na uwekezaji imeongezeka ikiwamo sekta ya utalii visiwani Zanzibar.

"Siku za nyuma wafanyabiashara waliokuwa wakileta bidhaa katika makontena walikuwa kati ya watano hadi sita lakini sasa zaidi ya wafanyabiashara 30 wanaingiza mizigo kutoka nje ya Zanzibar.

Aidha, alisema ujenzi wa Bandari ya Mangapwani itakapokamilika Zanzibar itafunguka kiuchumi na kuwa kituo cha biashara Afrika Mashariki.

Kuhusu mfumuko wa bei uliojitokeza umesababishwa na mambo manne kuibuka kwa maradhi ya ugonjwa wa virusi vya corona, ukame uliojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi na vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine.

"Siasa sio kila jambo kusema uongo, Zanzibar chakula kipo tena cha kutosha pamoja na uzalishaji wa mazao ya chakula na nafaka kuathiriwa duniani,"alisema Mbeto.

Alisema viongozi wa Chama cha ACT -Wazalendo walipaswa kumpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa maendeleo anayoendelea kuyaleta kwa muda mfupi baada ya kubeza juhudi zake.

Alisema katika kukabiliana na tatizo la mfumuko wa bei, serikali inatoa kila mwezi Sh. bilioni 21 kufidia kudhibiti ongezeko la bei ya mafuta ili kuleta unafuu kwa wananchi wa Zanzibar.

Aidha, alisema kwamba serikali inaendelea na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 275 ikiwamo barabara kuu na za ndani katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Kuhusu kero za muungano, alisema kamati ya pamoja imetatua kero 22 kati ya 25 na kuondoa malalamiko katika sekta mbalimbali za kiuchumi.



Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Khamis Mbeto, akionyesha ilani ya chama hicho, wakati akijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Chama cha ACT-Wazalendo kwenye mikutano ya hadhara, alipokutana na waandishi wa habari katika ofisi kuu ya CCM Kisiwandui jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Daktari bingwa awapa somo wenye matatizo ya hedhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

DAKTARI Bingwa wa Afya ya Uzazi kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk.Ummulkurthum Omar, amewataka wanawake walioﬁkia umri wa ukomo wa hedhi na bado wanaendelea kupata wawahi hospitali ili kuchunguzwa afya.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Alisema mwisho wa ukomo wa hedhi ni kati ya miaka 45 na 55 na mwanamke anapotokwa na hedhi zaidi ya muda huo huenda ikawa ni tatizo la kiafya, hivyo ni vyema kuwahi hospitali kuonana na wataalamu wa afya.

"Ukomo wa hedhi hufikia pale kutopata hedhi kwa muda wa miezi 12 mfululizo na unapofikia muda huo baadaye ikatoka hilo ni tatizo la kiafya na huenda ikawa ni tatizo la maradhi au magonjwa mengine,"alisema.

Daktari huyo alisema mwanamke anapofikia ukomo wa hedhi huwa hana uwezo tena wa kupata mtoto na uzazi huwa umefunga.

Alisema mwanamke anapofikia muda wa kukoma kwa hedhi hupata mabadiliko ya kibaiolojia ikiwamo kuongezeka uzito, ukavu katika sehemu za uke, kupata maumivu wakati wa tendo la ndoa na kuwa na hasira zaidi.

Aidha, aliwataka wanawake ambao uke wao ni mkavu na kuathiri ndoa zao kufika hospitali kuonana na wataalamu wa afya kwa ajili ya uchunguzi wa afya zao na kupata suluhisho ili kufurahia ndoa zao.

Alisema mwanamke anapofikia ukomo wa hedhi madini ya calcium mwilini hupungua, hivyo ni vyema kula vyakula vinavyotengeneza madini hayo na kula vyakula vyenye vitamini ikiwamo maziwa, mayai na kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi ili kuimarisha mwili.

Hata hivyo aliwataka wanawake kufanya uchunguzi wa afya zao ikiwamo saratani ya matiti na shingo ya kizazi ambayo inawaathiri sana wanawake.

# Watanzania wapewa hadhari ya kujikinga ugonjwa wa figo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Muhidini Abdi Mahmoud, amewataka wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa figo kwa sababu gharama za matibabu hayo ni ghali.

Dk.Muhidini ambaye ni Daktari Bingwa wa Figo alisema miongoni mwa tahadhari hizo ni kuacha kula vyakula vyenye mafuta mengi na vyenye kemikali na badala yake kula vyakula vyenje afya ikiwamo mboga, matunda na kufanya mazoezi.

Alisema utafiti uliofanyika kuhusu ugonjwa wa figo imeonyesha kwamba asilimia 10 ya idadi ya watu duniani wanasumbuliwa na ugonjwa wa figo na kati ya watu 100 kuna watu 10 wanatatizo hilo.

Alisema Zanzibar hakuna utafiti uliofanyika lakini idadi ya wagonjwa wa figo wapo wengi na kwa sasa inatoa huduma za kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo, kwamba kwa siku wagonjwa 40 wanahudumiwa.

"Tatizo la figo ni kubwa na wenye uhitaji ni wengi. Tanzania nzima inakadiriwa watu 8,500 wana uhitaji wa kupata huduma kuchuja damu kwa sababu ya matatizo ya figo na wameshafikia hatua ya mwisho, lakini wenye kupata huduma wapo 2,700,"alisema. Alisema ili kupunguza athari ya magonjwa hayo lazima jamii ipewe elimu ya umuhimu wa figo na namna ya kujikinga na athari za ugonjwa huo.

Alisema pia waathirika wa ugonjwa huo wanapaswa kuchukua hatua ili ugonjwa huo usifikie katika hatua ya mwisho ambayo itasababisha kupandikizwa figo au kuchuja sumu katika damu.

Dk. Muhidini alisema huduma ya kuchuja sumu katika damu kwa mgonjwa wa figo gharama yake ni Sh. 300,000 kwa huduma ya siku moja wakati mgonjwa mwenye uhitaji wa huduma hiyo hutakiwa ndani ya wiki moja kupata huduma kwa siku tatu.

Alisema figo ni kiungo muhimu kwa binadamu na kazi yake kuu ni kuchunja taka mwilini, hivyo zinaposhindwa kufanya kazi binadamu hupoteza maisha.

Alisema miongoni mwa visababishi vya ugonjwa wa figo ni mfumo mbaya wa maisha ikiwamo ulaji holela, utumiaji wa vyakula vya chumvi nyingi, shinikizo la damu, kisukari, utumiaji wa pombe, sigara, tumbaku na matumizi mabaya ya dawa za hospitali na miti shamba.

Hivyo aliitaka jamii kuwa na utamaduni wa kuchunguza afya zao mara kwa mara kwa sababu ugonjwa wa figo ukigundulika mapema unatibika. Meneja wa Kitengo cha Maradhi yasiyoambukiza Zanzibar, Dk. Omar Muhammed Suleiman, alisema maradhi ya figo ni sehemu ya maradhi yasiyoambukiza na wanahitaji kuwekeza zaidi katika kinga kwa sababu gharama za magonjwa hayo ni kubwa.

Hivyo alitaka jamii kubadilisha mfumo wa maisha kuacha kutumia vyombo vya moto vya usafiri kwa muda mrefu na mabadala yake kuwa na utamaduni wa kutembea ili kuimarisha kinga.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## PATA MKOPO KWA HARAKA

PATA MKOPO KWA HARAKA
**HADI 200,000,000/=**
KUTOKA
**ENTERPRISE FINANCE LIMITED**
KWAAJILI YA DHARURA MBALIMBALI KAMA KULIPA KODI YA NYUMBA, KUNUNUA GARI, KUBORESHA BIASHARA N.K

**TUNAPATIKANA**
DAR ES SALAAM **0677111333**
NA ARUSHA **0677226960.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ADAM SAID MAULID** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya TVS KING yenye usajili namba MC 809 AVE na CHASSIS NAMBA: MD6M14PK2F4E71917.kwa yeyote atakaeiona atoe tarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/R-B/87634/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA..........**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na 28 /20.....................**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CATHERINE MANGULA OGESSA KINGURUNYEMBE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA IGNAS ALEX MANGULA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo.
Tarehe 20 mwezi 3 mwaka 2023kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 3 mwaka 2023

HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI




**BYAMKAMA MULOKOZI ALIGAWESA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index No. S2506-0019 kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia CARMEL SECONDARY SCHOOL mwaka 2014.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/87925/2023.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**PETER GODFREY MGHASE** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 269400 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **KW/IRI/RB/797/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKSON BUNDALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S0367/0075 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KILOSA SEKONDARI mwaka 2000. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/87480/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILINDI**
**Kituo cha SONGE**
**Mkoa TANGA**
**Shauri la Madai/Ndoa 09/2020**
**Jina la Mdai.............HAMIDA STEWADI MGENI**
**Jina la Mdaiwa .......RAMADHANI ADAMU MOHAMEDI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa. RAMADHANI ADAMU MOHAMEDI**
Kwa kuwa Mdai ameleta..............MADAI YA MGAWANYO WA MALI ZA NDOA ..........
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe..15..Mwezi..03..Mwaka..2023.. Saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa Shauri hili ni lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu Shauri hili kwaajili ya kujitetea .
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa Shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza Shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe ...28...mwezi.. 02...mwaka...2023

.....................................
**HAKIMU**

FAHAMU:
Iwapo unafikiria kuwa Mashahidi wako hawatohudhuria kwa hiari yao wenyewe unaweza kupewa hati ya kuitwa Shaurini katika Mahakama hii ya kuwalazimisha mashahidi wote wahudhurie na kupeleka hati yoyote inayohitajiwa mbele ya Mahakama. Unaweza kuiomba Mahakama kwa kulipa ada ipasavyo.

## *OFISI ZA MATANGAZO*

*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042,*

*Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.*

*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*

*Website: www.ippmedia.com*


# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kimbunga Freddy kuipiga Msumbiji kwa mara ya pili

**MAPUTO, Msumbiji**

KIMBUNGA Freddy kinatarajiwa kuipiga tena Msumbiji wiki ijayo baada ya kuleta maafa nchini Madagascar jumatatu.

Serikali ya Madagascar ilisema watu wanane waliuawa na zaidi ya nyumba 1,000 ziliharibiwa.

Kimbunga hicho kilisababisha maafa kwa mara ya kwanza eneo hilo la kusini-mashariki mwa Afrika mwishoni mwa Februari, na kuua watu 21 na idadi kubwa ya watu kuhama makazi katika nchi zote mbili.

Wataalamu wa hali ya hewa wanasema ni nadra kuona kimbunga kukaa kwa muda mrefu kama hicho.

Kimbunga hicho cha kitropiki ambacho kinajiongeza nguvu kiko mbioni kuwa dhoruba ambayo imedumu muda mrefu zaidi kuwahi kurekodiwa.

Dhoruba hiyo tayari imevunja rekodi kwa kuwa na nguvu ya kutembea kilomita 8,000 kwa saa iliyopita katika Bahari ya Hindi.

Kutokana na kimbunga hicho kukaa muda mrefu na kuwa na nguvu, kimevutia wataalam wa hali ya hewa ulimwenguni kote kwa kutaka kujua zaidi.

Kimbunga hicho kilizuka katika Pwani ya kaskazini mwa Australia, mwanzoni mwa mwezi Februari na kisha kusafiri maelfu ya kilomita kuvuka kusini mwa Bahari ya Hindi, na kuathiri Mauritius na La Réunion, kabla ya kupiga nchini Madagascar na Msumbiji.

Wataalamu walisema hiyo ni njia nadra sana kupita kwa dhoruba kama hiyo.

Tayari kimbunga Freddy kinashikilia rekodi ya kusanyiko la juu la nishati ya inayounda kimbunga katika ukanda wa kusini.

Hata hivyo, kinatarajia kuipiga Msumbiji kwa mara ya pili, huku ikiwa taifa hilo bado linahangaika na mvua na mafuriko yaliyoletwa na kimbunga hicho.

Madagascar ilipata takriban mara tatu ya wastani wa mvua yake ya wastani ya kila mwezi katika wiki moja iliyopita.

Kamati ya tathmini ya Hali ya Hewa na Hali ya Hewa ya Umoja wa Mataifa, ilisema pengine itaanzisha uchunguzi kuhusu tukio hilo la ajabu na nadra baada ya kimbunga hicho kutoweka.

***BBC***



Wanajeshi wa Burkina Faso wakiwa katika opereshini ya kuwasaka waasi wanaoleta vurugu kaskazini mwa nchi hiyo. **PICHA: DW**

# Jeshi laua wanamgambo 110 Burkina Faso

WANAMGAMBO 110 wanaodaiwa kuwa magaidi wameuawa nchini Burkina Faso katika kipindi cha siku chache wakati serikali ikiendelea na operesheni kwa kutumia anga.

Operesheni hiyo inawalenga vikundi vya waasi vinavyoendesha harakati zao kaskazini na kusini mwa nchi hiyo.

Msemaji wa jeshi la nchi hiyo amethibitisha operesheni hiyo, bila kusema idadi kamili ya watu waliouawa mpaka sasa.

Upande wa kaskazini mwa Burkina Faso, amri ya kutotembea nje usiku na marufuku ya kuendesha aina fulani ya pikipiki imewekwa tangu wiki iliyopita.

Serikali ya mpito inayoongozwa na Rais Ibrahim Traore, ambayo iliingia madarakani kupitia mapinduzi ya kijeshi, mpaka sasa imeshindwa kuwarudisha nyuma wanamgambo hao.

Karibu askari 70 waliuawa katika mashambulizi ya Februari pekee. Kwa mujibu wa shirika la haki za binaadamu nchini humo la Burkina Faso Movement for Human and Peoples Rights, karibu raia 60 waliuawa wakati wapiganaji walikishambulia kijiji kimoja cha mkoa wa Tapoa mashariki mwa nchi hiyo.

***DW***

**Serikali ya mpito inayoongozwa na Rais Ibrahim Traore, ambayo iliingia madarakani kupitia mapinduzi ya kijeshi, mpaka sasa imeshindwa kuwarudisha nyuma wanamgambo hao.**

# Russia yadaiwa kupoteza wanajeshi 30,000 Bakhmut

**KYIV, Ukraine**

MAOFISA kutoka nchi za Magharibi wamesema kati ya wanajeshi 20,000 na 30,000 wa Russia wameuawa au kujeruhiwa katika vita vinavyoendelea kuwania mji wa Bakhmut nchini Ukraine.

Walisema idadi hiyo tangu mapigano hayo yaanze na kwamba kilele cha vita hiyo ya udhibiti wa jiji hilo haikuwa sawa kutokana na umuhimu wake mdogo wa kimkakati.

Baada ya zaidi ya miezi sita ya mapigano makali, hatima ya jiji hilo bado haijaamuliwa, na ni asilimia kumi tu ya wakazi wake bado waliosalia eneo hilo.

Mji huu mdogo, ulioko katika mkoa wa Donbass, umekuwa magofu na mabaki ya miti iliyoharibiwa na ukali wa mapigano.

Maofisa hao walisema kwamba Russia itapata mafanikio kidogo hata kama itachukua udhibiti wa mji huo kwa sababu imepoteza nguvu kubwa, na hadi kufikia lengo kunaweza kuchukua muda.

Serikali ya Ukraine, ilisema vita vya Bakhmut vilikuwa fursa adimu ya kuua Warusi wengi.

Jeshi la Ukraine pia limepata hasara kubwa, ingawa maofisa wa Magharibi wanapuuza takwimu zilizotajwa na Waziri wa Ulinzi wa Russia, Sergei Shoigu, katika hutuba yake ya juzi.

Shoigu alisema katika taarifa yake kwenye mkutano wa kijeshi, iliyochapishwa kwenye mtandao wa Telegram, kwamba Ukraine imepoteza wanajeshi 11,000 mwezi Februari pekee

Wakati huo huo, Ukraine imekanusha kuhusika kwa namna yoyote na shambulio dhidi ya mabomba ya gesi ya Nord Stream, lililotokea mwezi Septemba mwaka jana.

Ufafanuzi wa Ukraine unakuja baada ya ripoti ya gazeti la New York Times, ambao unawataja maofisa wa kijasusi wa Marekani kuvujisha siri kwamba kundi linalounga mkono nchi hiyo ndilo linalohusika.

Katika ripoti tofauti, vyombo vya habari vya Ujerumani vilisema wachunguzi wanaamini walitambua mashua iliyotumiwa kutega vilipuzi.

Usafirishaji wa gesi kupitia bomba ulikuwa umesitishwa kabla ya milipuko hiyo.

Russia ilifunga bomba la Nord Stream 1 , Agosti mwaka jana, ikidai linahitaji matengenezo. Bomba la Nord Stream 2 halijawahi kusafirisha gesi.

Sababu kamili ya milipuko iliyotokea na kupasua mabomba ya gesi asilia haijulikani, lakini inaaminika kuwa yalishambuliwa.

Russia imezilaumu nchi za Magharibi kwa milipuko hiyo na kutoa wito kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwachunguza.

Viongozi wa Nato na nchi za Magharibi wameacha kuishutumu Russia moja kwa moja, ingawa EU ilisema hapo awali kuwa Russia inatumia mabomba yake ya gesi kama silaha dhidi ya Magharibi.

***BBC***

## HABARI MICHEZO

# AZAM YAANZA KUCHANGA KARATA KUIKABILI IHEFU SC

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC kimeanza mazoezi rasmi kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu FC utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Highlands Estates ulioko Mbarali mkoani Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili, Msemaji wa Azam FC, Zakaria Thabit, 'Zaka', alisema baada ya mchezo uliopita wa mashindano ya Kombe la FA (ASFC), wachezaji walipewa mapumziko na jana wameanza rasmi maandalizi ya kuelekea mchezo huo.

Zaka alisema wanahitaji kikosi chao kiwe imara zaidi kwa sababu wanafahamu wenyeji wao wameimarika na hawataki kupoteza pointi wakiwa nyumbani.

Alisema wamejiandaa kukutana na ushindani katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu kwa kila upande.

"Kikosi kimeanza mazoezi rasmi leo (jana), kuelekea mchezo wetu dhidi ya Ihefu, tutakuwa ugenini na kikosi kitasafiri Jumapili ya Machi 12, mwaka huu, kuelekea Mbarali tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu kutoka kwenye mchezo huo," alisema Zaka.

Aliongeza malengo ya Azam ni kupata ushindi na kuhakikisha wanamaliza ligi hiyo wakiwa katika nafasi tatu kwenye msimamo wa ligi.

"Tunaenda kufuata pointi tatu, ingawa tunajua hakuna mechi rahisi, hivyo ni lazima tujiandae kupambana," Zaka aliongeza.

Alisema kila mchezaji wa timu hiyo anafahamu malengo waliyonayo kwa sasa baada ya kujiondoa kwenye mbio za kuwania taji hilo linaloshikiliwa na Yanga huku watani zao, Simba wakishika nafasi ya pili.

"Tunaupa umuhimu mkubwa mchezo huu na tumejiandaa kukutana na ushindani mkubwa, tunaenda kutafuta matokeo chanya, tumewaambia wachezaji wasibweteke na wasidharau wapinzani tunaokutana nao," ofisa huyo aliongeza.

Azam FC iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 47 sawa na Singida Big Stars wakati vinara ni mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 62 na Simba inafuatia ikiwa na alama 54.




Wanamichezo wenye ulemavu, Sophia Mbeyela (kushoto), Rehema Said (katikati) na Mwanaidi Ng'itu wakiwa na tuzo walizopata kutokana na mafanikio mbalimbali waliyopata ikiwa ni sehemu ya sherehe za Siku ya Wanawake Duniani iliyoandaliwa na Global Peace Foundation. Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA), Shamim Khan (katikati waliosimama), alikuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga Princess yafungua milango

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewataka wazazi na walezi ambao ni wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwapeleka mabinti zao wenye vipaji vya kucheza soka kujiunga na kikosi chao cha Yanga Princess inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, imeelezwa.

Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema hayo wakati akizungumza na wanachama na mashabiki wanawake wa timu hiyo jijini Dar es Salaam jana ikiwa ni kuadhibimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Mfikirwa alisema mpira wa miguu si wa wanaume peke yao, badala yake hata kinadada na kinamama wameonekana kuwa na vipaji vikubwa katika mchezo huo ambao kwa sasa umekuwa ni ajira kubwa.

"Kuna timu ya wanawake inaitwa Yanga Princess, inahitaji kuungwa mkono pia na nyinyi kinamama. Timu ile tumeianzisha kwa ajili ya kutoa fursa pia kwa wanawake kushiriki katika michezo na kama mnavyojua siku hizi mpira ni ajira," alisema Mfikirwa.

Aliwasisitiza wazazi kuwapeleka mabinti zao kufanya majaribio na watakaobainika kuwa na viwango watapata nafasi ya kusajiliwa kwenye kikosi cha timu hiyo.

"Kwa hiyo msione haya, msione tabu mkiona watoto wenu wa kike wana vipaji vya mpira, basi mjue klabu yenu inayo timu ambayo inasapoti kinamama na kinadada, tunaomba mjitokeze," aliongeza.

## ZFF yawaandalia wanawake darasa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), linajipanga kuendesha mafunzo mbalimbali kwa ajili ya wanawake ili kuwaandaa vyema ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea msimu ujao, imefahamika.

Katibu Mkuu wa (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema lengo la kuandaa mafunzo katika idara mbalimbali kwa wanawake ni kuwapa fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za soka huku wakiwa na weledi.

Vuai alisema kwa Zanzibar bado ushiriki wa wanawake katika soka uko chini ikilinganishwa na michezo mingine hivyo wanalazimika kuwahamasisha kwa kuwapeleka darasani.

Alitaja mafunzo ambayo yatatolewa kwa wanawake ni ya uamuzi, usimamizi wa mechi, ukamishna, uongozi na kuwaandaa watoto wa kike kufahamu namna ya kuokota mipira wakati mechi mbalimbali zinaendelea.

"Mpira wa miguu duniani kote hivi sasa umebadilika, wanawake wanashiriki kikamilifu katika masuala ya soka, lazima na sisi tuibadilishe jamii yetu hasa ya wanawake kushiriki na kuitumia fursa hii," Vuai aliongeza.

## Tanzania, India wafurahia kipekee

**Na Romana Mallya**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Kituo cha Utamaduni cha Swami Vivekananda (SVCC) , kimewakutanisha Watanzania na Wahindi kuimba nyimbo za Kihindi lengo la kuimarisha ushirikiano wa kitamaduni.

Maadhimisho hayo yaliyanyika jana katika kituo hicho na kuhudhuriwa na Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan huku nyimbo zaidi ya 17 ziliimbwa kwa kuwahusisha wasanii saba wa Watanzania ambao wanajifunza muziki katika kituo hicho.

Mkurugenzi wa SVCC, Dk. Soumya Chavan, alisema maadhimisho hayo yaliyojulikana kwa jina la 'An evening of Ghazals' yalilenga kuimarisha uhusiano wa kitamaduni na maelewano kati ya India na Tanzania.

"Tunapoadhimisha siku ya kimataifa ya wanawake tunafurahi sana kuona wanafunzi wanaosoma katika SVCC wamepata nafasi ya kuimba darasa la muziki wa Kihindi lililoendeshwa na TIC Vishnu Mishra," alisema Chavan.

Balozi Pradhan alisema tukio hilo linahimiza mabadilishano ya kitamaduni na kujenga urafiki kupitia sanaa na utamaduni.

## ZISIKUPITE

### CAICEDO AGOMBEWA SOKONI

ARSENAL, Manchester United, Chelsea na Liverpool bado zinavutiwa na Moises Caicedo licha ya kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ecuador mwenye umri wa miaka 21 kutia saini mkataba mpya na Brighton wiki iliyopita. ***(Football Insider)***

### OSIMHEN ATAJWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye mwe umri wa 24 na kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice (24), ndio wachezaji walengwa wakuu wa Arsenal msimu huu wa joto. ***(Sun)***

### BELLINGHAM, MADRID WATETA

MKUU wa Kitengo cha Uajiri wa Real Madrid, Juni Calafat, alifanya mkutano na babake kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 katika hoteli moja ya London, Jumanne. ***(Footmercato)***

### RABIOT AGOMBEWA ULAYA

LIVERPOOL, Manchester United na Tottenham Hotspur zimeomba kufahamishwa kuhusu hali ya mkataba wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 27 ambaye anaichezea Juventus ya Italia. ***(90Min)***

### MOUNT ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imejiunga kwenye mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Mason Mount ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### CITY YAMTAKA LAVIA

KLABU ya Manchester City ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Southampton baada ya kujumuisha kipengele cha kumnunua tena katika mkataba wake. ***(Football Insider)***

### LAPORTA, BABA MESSI WAKUTANA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, hivi majuzi alikutana na babake mshambuliaji wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi, na ameacha wazi uwezekano wa kurejea Nou Camp msimu wa joto kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35. ***(Goal)***

### LIVERPOOL YAMTAKA SILVA

LIVERPOOL na Tottenham Hotspur zilituma maskauti kuwatazama beki wa Benfica Mreno, Antonio Silva, mwenye umri wa miaka 19 na kiungo wa kati, Florentino Luis (23). ***(90min)***

### UNITED, WANUNUZI KIKAONI

MAZUNGUMZO kati ya Manchester United na wanunuzi wa klabu hiyo yataanza wiki hii, huku kundi la Qatar linaloongozwa na Sheikh Jassim bin Hamad Al Thani likifikiriwa kuwa mstari wa mbele. ***(Mail)***

### TIMBER NJIA PANDA

MLINZI wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Jurrien Timber, mwenye umri wa miaka 21 anayelengwa na Manchester United amesema atazingatia chaguo lake msimu huu wa joto. ***(Ajax Life, Via Mirror)***

### BRIGHTON, NICE VITANI

KLABU za Brighton na Nice zina nia ya kumsajili winga wa England, Reiss Nelson, mwenye umri wa miaka 23 baada ya mkataba wake na Arsenal utakapokamilika msimu huu wa joto. ***(CBS Sports)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# POTTER: CHELSEA SASA IMEBADILIKA

●●●Ni baada ya kuonyesha kiwango safi na kuiondoa Dortmund katika...

**LONDON, England**

KOCHA Graham Potter alikuwa mwenye hisia kali na alisifu uchezaji "mzuri" wa Chelsea baada ya kukata tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuwafunga Borussia Dortmund mabao 2-0 katika mchezo uliochezwa juzi usiku.

Mabao kutoka kwa Raheem Sterling na Kai Havertz yalipindua matokeo ya mchezo wa mkondo wa kwanza katika hatua ya 16 bora pale uliofanyika kwenye Uwanja wa Stamford Bridge.

Katika mchezo wa kwanza Chelsea ikiwa ugenini ilifungwa bao 1-0.

Ushindi huo wa mabao 2-0 uliwafanya Chelsea yenye makao makuu yake London Magharibi kupata ushindi wa pili mfululizo kwa mara ya kwanza tangu Oktoba, mwaka jana ikiwa imetoka kushinda mchezo wa Ligi Kuu England wikiendi iliyopita.

Potter mwenye umri wa miaka 47 alisema baada ya mechi: "Sina hakika jinsi ninavyohisi! Kuna hisia nyingi sana. Nilikuwa na wasiwasi, lakini walicheza vizuri."

"Nimefurahi kwa wao kupata ushindi na ni mzuri kwa kila mtu hapa.

"Kulikuwa na hisia nzuri kwenye chumba cha kubadilishia nguo. Tumepitia kipindi kigumu na mashindano haya yana maana kubwa kwetu.

"Tulitaka kusonga mbele na kuingia katika nafasi nane inatuweka sawa kwa wiki chache zijazo.

"Ni nzuri kwa wachezaji, ushindi wa mabao mawili ni safi baada ya kipindi kigumu. Unapata hilo maishani na ni jinsi unavyojibu na wachezaji wamekuwa wazuri.

"Hali ya kustaajabisha, jioni ya kustaajabisha, wachezaji walikuwa wazuri, mashabiki walikuwa wazuri.

"Walipaswa kuwa dhidi ya timu ambayo ilikuwa inafanya vizuri sana. Nadhani katika mechi mbili tulizostahili kupitia, ulikuwa usiku maalum."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,087,3

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
BETIS
1 | 1.46
X | 4.25
2 | 6.23

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# XAVI, BUSQUETS KUONGEZEWA MIKATABA

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, anataka kuwaongezea mikataba mipya, Xavi na Sergio Busquets ili kuongeza uhusiano wao wa muda mrefu na klabu hiyo.

Mchezaji wa zamani, Xavi sasa ni Kocha Mkuu wa Blaugrana hao huku Busquets akibaki kuwa sehemu muhimu ya safu yao ya kiungo kwani timu hiyo ya Katalunya ikiongoza msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa pointi tisa dhidi ya wapinzani wao Real Madrid.

Lakini kutokana na mkataba wa Busquets umemalizika mwishoni mwa msimu huu na ule wa Xavi ukiwa umebaki mwaka mmoja, kulikuwa na sintofahamu kuhusu ni muda gani magwiji wa klabu hiyo watakaa hapo Camp Nou.

Hata hivyo, Laporta alifafanua hali hiyo na kufichua klabu hiyo iko tayari kutoa mikataba mipya kwa wawili hao.

"Tayari nimefikiria juu ya kuwapa mikataba mipya," alisema Laporta akiwaambia waandishi wa habari.

"Nadhani tunapaswa kumpa mkataba mpya Xavi kwa sababu anastahili.

"Anaijua nyumba hii vizuri zaidi. Anaijua Barca na anaielewa vyema hali ya klabu.

"Tumezungumza kuhusu Busquets. Yeye ni muhimu kwenye chumba cha kubadilishia nguo, ana namna ya kucheza inayoendana na mfumo wetu. Xavi anataka aendelee.

# Bellingham: Ni penalti ya mzaha

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, aliita penalti iliyorudiwa na Chelsea, ambayo iliiondoa timu yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne kuwa ni "mzaha."

Mechi hiyo ya mkondo wa pili wa hatua ya 16 bora kwenye Uwanja wa Stamford Bridge ilionekana kama ingekuwa sare baada ya The Blues hao kushinda bao 1-0 kupitia kwa Raheem Sterling.

Na hivyo ilimaanisha timu hizo zimepata sare ya 1-1 kwa ujumla baada ya mchezo wa kwanza Dortmund kushinda 1-0 nyumbani.

Lakini krosi ya Ben Chilwell ilionekana kugonga mkono wa Marius Wolf mapema kipindi cha pili.

Mwamuzi, Danny Makkelle akisaidiwa na Ofisa wa VAR, Pol Van Boekel, walikagua tukio hilo na baadaye akatoa mkwaju wa penalti ambayo Kai Havertz, alikosa kwa kugonga mwamba.

Hata hivyo, tathmini nyingine ya VAR iligundua wachezaji kadhaa wa Dortmund walikuwa wamevamia eneo la hatari kabla ya Havertz kupiga mpira na hivyo kumfanya Makkelle kuamuru ipigwe tena, na Mjerumani akafunga na kuipeleka timu yake robo fainali kwa jumla ya ushindi wa mabao 2-1.



## HABARI MICHEZO

305,640/-

# MOBBY ALIKUWA ALAMA KATIKA SOKA SHINYANGA

**Na Adam Fungamwango**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Shinyanga (SHIREFA), kimesema kilikuwa kinamtumia aliyekuwa mchezaji wa Mtibwa Sugar, marehemu, Iddi Mobby, kutangaza na kuhamasisha mchezo wa mpira wa miguu mkoani humo.

Mobby aliyefariki Jumapili iliyopita alizikwa juzi kwenye makaburi ya Mshikamano yaliyoko kwenye Kata ya Ndembezi, Shinyanga.

Mwenyekiti wa SHIREFA, Said Mankiligo, alisema Shinyanga imepoteza mtu muhimu katika tasnia hiyo kwa sababu alichangia kuwafanya wachezaji wenye vipaji kuupenda mchezo huo.

Mankiligo alisema walimtumia marehemu kutambua vipaji vilivyolala vijijini na walifanikiwa sana katika mchakato huo.

"Hili ni pengo kubwa sana kwa pande zote, taifa na klabu yake ya Mtibwa Sugar, sasa Mobby ameondoka, itabidi tufanye kazi ya ziada kuwarudisha vijana kwenye morali yao ili waendelee na kufika pale ambapo marehemu alifikia," alisema kiongozi huyo.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo alisema marehemu ameacha pengo katika familia yake, klabu na taifa kwa ujumla kwa sababu aliwahi kuitumikia timu ya taifa (Taifa Stars).

Mbali na Mtibwa Sugar, marehemu amewahi kuichezea timu mbalimbali za Ligi Kuu Bara zikiwamo Stand United, Polisi Morogoro, Polisi Tanzania, Mwadui FC na Ruvu Shooting.



Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (kushoto), akiwa amemkumbatia kiungo wa timu hiyo, Salum Abubakari 'Sure Boy' baada ya kumaliza mazishi ya mtoto wa nyota huyo aliyefariki juzi na kuzikwa kwenye makaburi ya Magomeni, Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

# CHANETA yawaamsha wanawake

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimewataka wanawake kutojiweka nyuma katika shughuli za michezo zinazofanyika kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kusaidia kuimarisha afya zao.

Kauli hiyo ya CHANETA imetolewa katika kusheherekea Siku ya Wanawake Duniani ambayo iliadhimishwa sehemu mbalimbali jana.

Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, aliliambia gazeti hili mwanamke ana ujasiri wa kufanya jambo lolote endapo atakuwa na nia na kwa sababu hiyo wanatakiwa kujiamini.

"Wanawake tunaweza, tusijiweke nyuma katika michezo, tunapaswa kujituma na kuonyesha tunaweza kufanya jambo lolote litakalotuletea heshima na kujitangaza, " alisema Marwa.

Aliongeza mwanamke ana uwezo wa kufanya shughuli yoyote ya kujiongezea kipato bila kumtegemea mwanaume jambo ambalo litamsaidia kujihudumia vizuri.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/03/23 | 18:00 | Everton FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 11/03/23 | 18:00 | Preston North End vs Cardiff City | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 03. 11/03/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Watford FC | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 04. 11/03/23 | 18:15 | Elche CF vs Real Valladolid | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 05. 11/03/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs Santa Clara Azores | 2.31 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 11/03/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KV Oostende | 2.46 | 3.30 | 2.60 |
| 07. 11/03/23 | 22:45 | Bologna FC vs Lazio Rome | 2.95 | 3.15 | 2.29 |
| 08. 11/03/23 | 23:00 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 09. 12/03/23 | 14:15 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.45 | 3.20 | 2.70 |
| 10 12/03/23 | 14:30 | US Lecce vs Torino FC | 2.85 | 2.90 | 2.55 |
| 11. 12/03/23 | 16:00 | RCD Mallorca vs Real Sociedad San Sebastian | 3.20 | 2.85 | 2.36 |
| 12. 12/03/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs Montpellier HSC | 2.75 | 3.10 | 2.50 |
| 13. 12/03/23 | 17:00 | FC Nantes vs OGC Nice | 3.05 | 3.10 | 2.28 |
| 14. 12/03/23 | 17:00 | Hellas Verona vs AC Monza | 2.36 | 3.05 | 2.95 |
| 15. 12/03/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs Gil Vicente Barcelos | 2.28 | 3.10 | 3.05 |
| 16. 12/03/23 | 20:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.29 | 3.40 | 3.05 |
| 17. 12/03/23 | 21:30 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.26 | 3.20 | 3.30 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 09/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3095 | Aktobe vs Okzhetpes | 1.43 | 3.90 | 6.57 |
| 13:00 | 3930 | PS Tni vs PSM Makassar | 3.19 | 3.08 | 2.12 |
| 14:00 | 2619 | Rio Ave U23 vs Leixoes SC U23 | 2.05 | 3.27 | 3.27 |
| 14:30 | 5495 | Bandirmaspor vs Eyupspor | 2.93 | 3.24 | 2.18 |
| 14:45 | 4851 | Albirex Niigata (SIN) vs Lion City Sailors | 2.08 | 3.34 | 3.03 |
| 14:45 | 5196 | Young Lions vs Tampines | 9.63 | 6.35 | 1.18 |
| 15:00 | 2582 | Aksu vs Kairat Almaty | 2.88 | 3.19 | 2.22 |
| 15:00 | 3126 | Saudi Arabia U20 vs Japan U20 | 3.42 | 3.27 | 1.99 |
| 15:00 | 5678 | KF Ballkani vs KF Drita | 2.11 | 2.93 | 3.39 |
| 16:00 | 1028 | AL Baten vs Al Khaleej Club | 4.20 | 3.72 | 1.78 |
| 16:00 | 3172 | KMC vs Kagera Sugar | 2.26 | 2.80 | 3.24 |
| 16:00 | 5550 | Al-Ettifaq vs Al Wehda | 1.95 | 3.30 | 3.10 |
| 16:30 | 1128 | NK Bistrica vs ASK Bravo | 5.08 | 4.36 | 1.48 |
| 17:00 | 2621 | Hyderabad FC vs ATK Mohun Bagan | 2.35 | 3.32 | 2.61 |
| 18:00 | 1149 | Sporting CP U23 vs Portimonense U23 | 2.43 | 3.47 | 2.50 |
| 18:20 | 3030 | Al Salmiyah vs Al Kuwait SC | 4.51 | 3.54 | 1.65 |
| 18:20 | 3415 | Al Jahra vs Al Fehaheel | 2.62 | 3.29 | 2.35 |
| 18:30 | 2181 | East Riffa vs Sitra Club | 3.11 | 2.95 | 2.28 |
| 18:30 | 2453 | Al Nahda (Oman) vs Al Seeb | 2.45 | 2.65 | 2.85 |
| 18:30 | 2815 | AL Badii vs Muharraq SC | 10.38 | 4.98 | 1.25 |
| 19:00 | 1815 | JK Tammeka Tartu II vs JK Narva Trans | 1.85 | 3.55 | 3.15 |
| 19:00 | 2913 | Laanemaa JK Haapsalu vs JK Welco Elekter | 3.11 | 4.25 | 1.84 |
| 19:00 | 4029 | Paide Linnameeskond vs FC Elva | 4.36 | 4.58 | 1.61 |
| 20:00 | 1014 | Viimsi JK vs Flora II | 1.88 | 3.99 | 3.46 |
| 20:00 | 1931 | VfB Lubeck vs Werder Bremen II | 1.56 | 4.00 | 4.78 |
| 20:00 | 3960 | Sakaryaspor vs Samsunspor | 3.19 | 3.35 | 2.01 |
| 20:30 | 2400 | Al Ittihad Jeddah vs Al Nasr Riyadh | 3.14 | 3.51 | 2.14 |
| 20:30 | 3135 | Al Shabab Riyadh vs AL Faiha | 1.61 | 3.84 | 5.33 |
| 20:30 | 5749 | CA Osasuna W vs Athletic Bilbao W | 3.99 | 3.99 | 1.67 |
| 20:45 | 1576 | AEK Larnaca vs West Ham | 4.84 | 3.83 | 1.63 |
| 20:45 | 3494 | El Fahem vs Maccabi Petach Tikva | 2.69 | 3.06 | 2.63 |
| 20:45 | 3513 | Sheriff Tiraspol vs Nice | 4.24 | 3.38 | 1.83 |
| 20:45 | 4166 | Union Berlin vs Union Saint Gilloise | 1.64 | 3.59 | 5.25 |
| 20:45 | 4209 | Anderlecht vs Villarreal | 3.48 | 3.38 | 2.01 |
| 20:45 | 4455 | Roma vs Real Sociedad | 2.12 | 3.03 | 3.59 |
| 20:45 | 4710 | Bayer Leverkusen vs Ferencvaros TC | 1.29 | 5.25 | 8.68 |
| 20:45 | 5268 | Sporting Lisbon vs Arsenal | 3.28 | 3.23 | 2.15 |
| 21:00 | 3663 | FC Tallinn vs JK Tabasalu | 1.77 | 3.70 | 3.30 |
| 21:30 | 2834 | Nova Iguacu RJ vs Madureira RJ | 2.17 | 2.96 | 3.32 |
| 21:30 | 5413 | Floresta CE vs Tiradentes CE | 1.61 | 3.42 | 5.39 |
| 22:00 | 4446 | HK Kopavogs vs IF Vestri | 1.26 | 5.60 | 7.67 |
| 23:00 | 1560 | FC Basel vs Slovan Bratislava | 1.81 | 3.58 | 4.04 |
| 23:00 | 2531 | Orsomarso vs Leones FC | 2.70 | 3.07 | 2.47 |
| 23:00 | 2638 | Sevilla FC vs Fenerbahce | 1.76 | 3.64 | 4.24 |
| 23:00 | 3760 | Fiorentina vs Sivasspor | 1.31 | 4.94 | 8.68 |
| 23:00 | 3830 | Juventus vs SC Freiburg | 1.70 | 3.42 | 5.01 |
| 23:00 | 4192 | KAA Gent vs Basaksehir | 2.03 | 3.33 | 3.48 |
| 23:00 | 4374 | Manchester Utd vs Betis | 1.46 | 4.25 | 6.23 |
| 23:00 | 5691 | Lech Poznan vs Djurgardens IF | 1.94 | 3.48 | 3.63 |
| 23:00 | 5958 | Shakhtar Donetsk vs Feyenoord | 2.93 | 3.44 | 2.23 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Machi 9, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## Potter: Chelsea sasa imebadilika



Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' (kushoto), akimkabidhi nahodha wa Simba, John Bocco, kiasi cha Sh. milioni tano kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Vipers FC katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SIMBA SC**

## Kocha mpya Stars awaita mashabiki

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA mpya wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Adel Amrouche, amewataka mashabiki wa soka kutoka sehemu mbalimbali nchini kumpa ushirikiano mkubwa ili afanye vizuri kazi yake ya kukinoa kikosi hicho.

Amrouche ametambulishwa rasmi na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pindi Chana jijini Dodoma juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Amrouche, alisema anaamini mashabiki wana nafasi kubwa katika maendeleo ya Taifa Stars na si kuwatisha wapinzani pale timu hiyo inapokuwa uwanjani.

"Kitu kikubwa na muhimu kwangu ni mashabiki, nataka mashabiki kutoka Kusini, Kaskazini na sehemu zote za Tanzania kunipa ushirikiano, tukiwa pamoja tutapata mafanikio, mashabiki huwaongezea nguvu wachezaji," alisema Amrouche.

Alisema kitu kingine anachoamini kitasaidia Tanzania kutimiza ndoto zake ni kuwapa nafasi wachezaji vijana na kwa kufanya hivyo, itasaidia kulinda na kuendeleza vipaji vya chipukizi hao.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema kocha huyo amepewa mkataba wa miaka mitatu na atasaidiwa na Hemed Suleiman 'Morocco'.

Amrouche ambaye ni raia wa Algeria na Ubelgiji, amewahi kufundisha timu za Taifa za Burundi, Botswana, Libya, Equatorial Guinea na Kenya ambayo aliweka rekodi ya kucheza mechi 20 bila kufungwa.

# SIMBA KUBADILISHA GIA

### Kocha akiri haikucheza vizuri, lakini ndoto za kutinga robo fainali...

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kupata ushindi na kufufua matumaini ya kusonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayoendelea, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amesema bado anahitaji muda wa kukisuka vyema kikosi chake ili kiwe imara hasa kwenye safu ya ushambuliaji.

Simba iliyopata ushindi wa ugenini na nyumbani dhidi ya Vipers FC ya Uganda, sasa imefikisha pointi sita na kukwea hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Kundi C ambalo linaongozwa na Raja Casablanca ya Morocco yenye pointi 12.

Horoya AC ya Guinea yenye pointi nne iko katika nafasi ya tatu huku Vipers SC inayoshika mkia kwenye kundi hilo katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ina pointi moja mkononi.

Simba itashuka tena dimbani katika michuano hiyo Machi 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuwakaribisha Horoya AC.

Akizungumza baada ya mchezo dhidi ya Vipers, Robertinho alisema pamoja kupata ushindi, mechi hiyo ilikuwa ngumu kwao na walicheza kwa nguvu kwa sababu walihitaji zaidi kuzipakisha pointi tatu nyumbani.

Robertinho alisema lengo lao kubwa lilikuwa ni kupambana kusaka ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye kundi lao. "Ulikuwa mchezo mgumu sana na hii ni kutokana na wapinzani wetu Vipers kutumia mashambulizi ya kushtukiza, lakini nafurahi lengo letu la kupata pointi tatu limetimia, ninawapongeza wachezaji wangu kwa hilo," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema presha ya uhitaji wa matokeo iliwasumbua wachezaji wake na kusababisha kushindwa kuzitumia vizuri nafasi nyingi walizitengeneza katika mchezo huo.

Aliongeza bado anahitaji muda wa kuendelea kuijenga timu hiyo ili icheze soka safi na la kuvutia huku ikipata ushindi mnono katika mechi za mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

Alisema muda wa miezi miwili au mitatu tangu alipokabidhiwa timu hiyo haitoshi kitaalamu kujenga kila kitu na kwa ukubwa wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo kipaumbele chake ni kuvuna pointi tatu.

"Sio kazi ya wiki moja au mbili kupandikiza mifumo na falsafa zangu kwa siku chache ambazo nipo hapa ukizingatia hatuna muda mrefu wa kufanya mazoezi, timu iko katika mashindano matatu tofauti, kila baada ya siku mbili au tatu tunacheza mechi hivyo mashabiki wanapaswa kutupa muda, hata hivyo nawapongeza wachezaji wangu kwa juhudi wanazozionyesha," alisema Robertinho.

Naye Kocha Mkuu wa Vipers, Roberto Luiz Bianch, amekiri kipigo hicho kimepoteza matumaini waliyokuwa nayo ya kufanya vizuri katika michuano hiyo Ligi ya Mabingwa Afrika.

Bianch alisema safu yake ya ushambuliaji ilikosa umakini na kushindwa kuzitumia vizuri nafasi nyingi za mabao walizotengeneza ndani ya mchezo huo na kupelekea kuwapa wenyeji ushindi.

"Nahisi huzuni sababu matokeo ya leo (juzi), yameyeyusha ndoto zetu za kufanya vizuri katika hatua hii ya mashindano, mchezo huu hatukustahili kupoteza, tungepata pointi tatu au hata sare, lakini tatizo lilikuwa kwa washambuliaji wetu," alisema Bianchi.

Wakati huo huo, Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA', juzi alikabidhi kiasi cha Sh. milioni tano kutoka kwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan kutokana na ushindi huo.

"Tunashukuru Mungu kwa kupata ushindi huu umuhimu ambao umetuweka katika nafasi nzuri, tunamshukuru Rais kwa zawadi hii ambayo inatuongezea morali. Tunaishukuru wizara ya michezo kwa sapoti mnayotupa, wachezaji tunapambana kwa ajili ya Simba na nchi kwa ujumla," alisema John Bocco, nahodha wa Simba baada ya kupokea fedha hizo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >